

**ATHARI ZA KIMOFOFONOLOJIA ZA KIOLUSUBA
KATIKA MATUMIZI YA KISWAHILI SANIFU KAMA
LUGHA YA PILI**

MEROLYNE ACHIENG OTIENDE

Tasnifu hii imewasilishwa kwa ajili ya kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada ya uzamili ya Kiswahili katika chuo kikuu cha Nairobi.

(2013)

UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa kwa mahitaji ya Digrii katika chuo kingine.

(Mtahiniwa)

Tarehe: _____

Merolyne Achieng Otiende

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa kazi hii.

Dkt. Iribe Mwangi

Tarehe: _____

Bi. Mary Ndungu

Tarehe: _____

(Wasimamizi)

TABARUKU

Naitabaruku kazi hii kwa mume wangu mpendwa Paul Rabala Oloo kwa imani aliyo nayo katika uwezo wangu. Pia kwa vito vya maisha yangu Wren, Avyn na Valene kwa kunihimiza kutia bidii.

SHUKRANI

Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuyakamilisha masomo yangu ya uzamili na pia kuikamilisha kazi hii. Hakika kazi kama hii haiwezi kukamilika bila msaada wa wengine. Ningependa kuzitoa shukrani zangu za dhati kwa wote waliochangia kwa njia moja au nyingine katika ufanisi wa utafiti huu. Kwanza kabisa nawashukuru wasimamizi wangu Dkt. Iribe Mwangi na Bi. Mary Ndungu ambao waliongoza kutoka mwanzo hadi nilipoikamilisha kazi hii. Daima nitawashukururu na kuwatakieni kheri na baraka zake Mtorehemezi.

Pili, nawashukuru walimu wangu wote. Aidha namshukuru Prof. Okoth Okombo kwa mawaidha aliyonipa mwanzoni mwa utafiti huu.

Vile vile nawashukuru walimu wa shule za msingi za Uozi, Wakinga na Gethsemane kwa kuniruhusu kutangamana na wanafunzi wao na kupata baadhi ya data iliyofanikisha utafiti huu. Hali kadhalika nawashukuru watangazaji wa kituo cha redio cha *Ekialo Kiona* wakiongozwa na Bonfas Msaswa kwa maelezo ya kina waliyonipa kuhusu masuala mbalimbali ya Kiolusuba. Sitamhini shukrani zangu mzee Fabian Ouma aliyenieleza mambo kadhaa kuhusu data ya utafiti huu.

Siwezi kuwasahau wanafunzi wenzangu tulioabiri nao chombo hiki kwa kunitia moyo kila mwendo ulipoonekana kuwa mgumu. Hao ni pamoja na Lily Chebet, Lydia Moraa, Grace Kanyua, Juliet Okeyo na Francis Onyonka.

Shukrani za kipekee kwa mume wangu Paul Rabala Oloo ambaye amekuwa katika mstari wa mbele kunihimiza kulenga juu masomoni na pia kunifadhili kwa hali na mali kuhakikisha nimefaulu. Pia, sitawasahau wanangu Wren, Avyn na Valene kwa subira waliyokuwa nayo na kuvumilia upweke wa ‘mama asiyekuwepo’ kila nilipowaacha na kwenda maktabani.

Ninajua kuna wengi waliochangia ambao sijawataja kwa ukosefu wa muda . Kwenu nyote nasema. Ahsante.

ISHARA NA VIFUPISHO VILIVYOTUMIKA

[]	Mabano ya fonimu
//	Mabano ya fonetiki
{ }	Mabano ya mofu
+	Mpaka wa mofu
\$	Mpaka wa silabi
#	Mpaka wa neno
→	Inabadilika na kuwa
I	Irabu
L ₁	Lugha ya kwanza
L ₂	Lugha ya pili
FZ	Fonolojia Zalishi
NFZA	Nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia
Kip	Kipasuo
Kons	Konsonanti
Naz	Nazali
Kiz-kikw	Kizuiwa kikwamizwa
Mh	Mhariri
Mid-meno	Midomo na meno

IKISIRI

Utafiti huu una lengo la kuchanganua athari za kimofonolojia za Kiolusuba katika matumizi ya Kiswahili Sanifu kama lugha ya pili. Utafiti huu umetumia nadharia ya FZA kuchambulia miundo ya lugha hizi mbili ili kuweka bayana athari hizo.

Sura ya kwanza ni muhtasari wa jinsi utafiti huu ulikavyofanywa. Imeshughulikia utangulizi, madhumuni, nadharia tete, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka, yaliyoandikwa kuhusu mada hii, msingi wa nadharia na njia za utafiti.

Sura ya pili imeshughulikia ulinganishi wa mifumo kamili ya fonimu za Kiswahili na Kiolusuba huku ikionyesha sifa bainifu za fonimu hizo. Aidha tumetoa mifano ya maneno yanayoundwa na fonimu hizo. Katika sura ya tatu, tumelinganisha na kulinganua miundo ya silabi katika Kiswahili na Kiolusuba.

Katika sura ya nne, tumeshughulikia mambo mawili. Kwanza, tumeziorodhesha ngeli za nomino za Kiolusuba. Kisha, tumeshughulikia mifanyiko ya kifonolojia inayohusu irabu na konsonanti za lugha hizi mbili huku tukionyesha peo za mifanyiko hiyo.

Data ya maneno yanayoonyesha baadhi ya athari za kisauti za Kiolusuba katika Kiswahili Sanifu imechanganuliwa katika sura ya tano. Maumbo sahihi yameonyeshwa huku maelezo yakitolewa kuhusu athari zenyewe.

Katika sura ya sita tumetoa hitimisho pamoja na matokeo ya utafiti huu kwa muhtasari. Mwisho, tumetoa maoni na mapedekezo kuhusiana utafiti huu.

YALIYOMO

Ungamo.....	ii
Tabaruku	iii
Shukrani	iv
Ishara na Vifupisho	v
Muhtasari	vi
Yaliyomo	vii
1. SURA YA KWANZA	1
1.1 Utangulizi	1
1.2 Tatizo la utafiti.....	3
1.3 Madhumuni ya utafiti	5
1.4 Nadharia tete.....	5
1.5 Sababu za Kuchagua Mada Hii.....	6
1.6 Upeo na mipaka	6
1.7 Yaliyoandikwa kuhusu somo hili	7
1.7.1 Yaliyoandikwa kuhusu athari za L_1 kwa L_2	7
1.7.2 Yaliyoandikwa kuhusu mofofonolojia za lugha nyingine zikilinganishwa na Kiswahili.....	9
1.7.3 Yaliyoandikwa kuhusu fonolojia na mofolojia za lugha mbalimbali	9
1.8 Msingi wa nadharia.....	10
1.8.1 Sheria za Kifonetiki	12
1.8.2 Sheria za Mofolojia ‘Mp’	13
1.8.3 Kanuni za Via.....	13
1.8.4 Sheria za Sandhi.....	14
1.9 Njia za utafiti	14
1.9.1 Utangulizi.....	14
1.9.2 Uteuzi wa sampuli.....	15
1.9.3 Mbinu za ukusanyaji data	15
1.9.4 Mbinu za uchanganuzi wa data	16
1.9.5 Njia za uwasilishaji wa data.....	16
1.10 Hitimisho	16
2. SURA YA PILI	17
2.1 FONIMU ZA KISWAHILI SANIFU NA KIOLUSUBA.....	17
2.1.1 Utangulizi.....	17
2.1.2 Fonimu za Kiswahili Sanifu.....	17
2.2 Fonimu za Kiolusuba.....	24
2.2.1 Fonimu za irabu za Kiolusuba	24
2.2.2 Konsonanti za Kiolusuba	27
2.2.3 Sifa bainifu za fonimu za Kiolusuba.....	30
2.3 Hitimisho	33

3. SURA YA TATU	34
3.1 MUUNDO WA SILABI KATIKA KISWAHILI NA KIOLUSUBA	34
3.1.1 Utangulizi.....	34
3.1.2 Muundo wa silabi katika Kiswahili Sanifu	35
3.1.3 Muundo wa silabi katika Kiolusuba.....	38
3.1.4 Ulinganishi na ulinganuzi wa miundo ya silabi za Kiswahili Sanifu na Kiolusuba.....	41
3.1.5 Ulinganuzi wa miundo ya silabi katika Kiolusuba na Kiswahili Sanifu....	43
3.2 Hitimisho	44
4. SURA YA NNE	45
4.1 NOMINO NGELI ZA KISWAHILI SANIFU NA KIOLUSUBA	45
4.1.1 Utangulizi.....	45
4.1.2 Ulinganishi wa mifanyiko ya kimofonolojia katika Kiswahili na Kiolusuba.....	57
4.1.3 Mifanyiko ya kimofonolojia ya irabu	59
4.1.4 Mifanyiko ya kimofonolojia ya konsonanti za Kiswahili na Kiolusuba	71
4.2 Hitimisho	78
5. SURA YA TANO	80
5.1 ATHARI ZA KIMOFOFONOLOJIA	80
5.1.1 Utangulizi.....	80
5.1.2 Athari katika matumizi ya /h/.....	81
5.1.3 Athari katika matumizi ya /ð/.....	81
5.1.4 Kubadilisha /x/ na /g/	81
5.1.5 Matumizi ya /s/ badala ya /ʃ/	82
5.1.6 Matumizi ya /j/ badala ya /tʃ/	82
5.1.7 Matumizi ya /s/ badala ya /θ/	83
5.1.8 Matumizi ya /k/ badala ya /x/.....	83
5.1.9 Uchopekaji wa irabu /u/	84
5.2 Hitimisho	87
6. SURA YA SITA	88
6.1 MATOKEO NA MAPENDEKEZO.....	88
6.1.1 Utangulizi.....	88
6.1.2 Muhtasari wa matokeo	88
6.1.3 Mapendekezo	89
MAREJELEO.....	90
VIAMBATISHI	93

ORODHA YA VIELELEZO

1.1	<i>Asili ya Kiolusuba.....</i>	2
2.1	<i>Fonimu za Irabu za Kiswahili Sanifu</i>	19
2.2	<i>Jedwali la irabu za Kiswahili Sanifu.....</i>	19
2.3	<i>Jedwali la Konsonanti zaKiswahili Sanifu</i>	24
2.4	<i>Irabu za Kiolusuba</i>	26
2.5	<i>Matriki ya irabu za Kiolusuba.....</i>	27
2.6	<i>Konsonanti za Kiolusuba.....</i>	32
4.1	<i>Jedwali la ngeli za Kiolusuba.....</i>	49
4.2	<i>Kuimarika kwa konsonanti</i>	75
5.1	<i>Athari katika kazi andishi</i>	85
5.2	<i>Baa grafu ya athari katika kazi andishi.....</i>	86
5.3	<i>Athari katika matamshi.....</i>	86
5.4	<i>Baa grafu ya athari katika kazi andishi.....</i>	87

1. SURA YA KWANZA


1.1 Utangulizi

Utafiti huu unahusu athari za kimofonolojia za Kiolusuba katika matumizi ya Kiswahili Sanifu kama lugha ya pili. Kiolusuba ni mojawapo kati ya lahaja za Kibasuba lugha ambayo inazungumzwa na Wabasuba jamii inayoishi katika visiwa na ufuo wa Magharibi mwa Ziwa Viktoria katika Jimbo la Homa-Bay. Kulingana na Mattah (2008), lugha hii ni ya asili ya Kibantu ambayo wazungumzaji wake walihamia nchini Kenya kama wakimbizi kutoka Uganda katika miaka ya mwisho wa Karne ya 18. Mchango wa Mattah umesawiana na wa Ayot (1973) ambaye pia anaeleza jinsi Wabasuba walivyovuka Ziwa Viktoria kwa mitumbi na kuanza kuishi kwenye ufuo wa ziwa hili katika sehemu za Gwasi na Kaksingri. Wataalamu ambao wamewahi kushughulikia lugha hii ni pamoja na Okombo na Rottland (1981) ambao walichunguza jinsi lugha hii ilivyoathirika kutokana na lugha jirani. Walitaja maeneo ambayo lugha hii huzungumzwa yakiwa ni pamoja na visiwa vya Mfangano, Remba, Takawiri na Rusinga miongoni mwa vingine.

Kazi za Guthrie (1947-67, 1970/71), Nurse (1985) na Greenberg (1966) zinaonyesha kwamba barani Afrika mna makundi manne makuu ya lugha nayo ni: *Niger-Kordofanian*, *Nile-Saharan*, *Afro-Asiatic* na *Khoisan*. Lugha za Kibantu ni miongoni mwa lugha katika kundi la *Niger-Kordofanian*. Lugha hizi huzungumzwa hasa kwenye maeneo ya Afrika ya kati na Mashariki. Nchini Kenya, lugha za Kibantu zimeainishwa katika makundi mawili makuu kimaeneo. Kuna lugha za Kibantu za maeneo ya Magharibi mwa nchi na za maeneo ya Mashariki mwa nchi. Osogo (1971) anasema kuwa Kibasuba ni lugha inayoorodheshwa katika kundi la zile za Magharibi mwa Kenya ikiwa na ukuruba sana na lugha nyingine kama Ekegusii, Kikuria na lahaja za Kiluhya.

Lugha ya Kibasuba ina lahaja tatu kuu kama ilivyoonyeshwa katika mchoro 1.1. Kuna lahaja ya Ekisuva inayozungumzwa kwenye maeneo ya Gwasi; lahaja ya Ekikune inayozungumzwa sehemu za Kaksingri na lahaja ya Kiolusuba inayozungumzwa

katika kisiwa cha Mfangano. Katika kazi hii tutarejelea Kiolusuba kwani ndiyo lahaja sanifu. Sababu kuu ni kwamba hata Biblia takatifu ya Kibasuba imeandikwa kwa lahaja hii.



Kielelezo 1.1 Asili ya Kiolusuba (Mchoro huu umebuniwa kutokana na Iribemwangi (2010)

Kwa upande mwingine tutaangazia Kiswahili Sanifu kwani ndiyo lugha tunayolenga katika utafiti huu ili kubaini jinsi inavyoathirika na matumizi ya Kiolusuba hasa kwa kuzingatia matumizi yake miongoni mwa wazungumzaji wa Kiolusuba. Kulingana na Guthrie (1971), Kiswahili ni lugha ya Kibantu. Nchini Kenya, lugha hii imeanishwa katika kundi la lugha za Kibantu za Pwani mwa nchi.

Sifa moja kuu inayozitambulisha lugha za Kibantu ni kwamba nomino zake hupangwa kwenye makundi yanayoitwa ngeli na ambayo katika sentensi huonyesha upatanifu wa kisarufi. Kwa mfano katika Kiswahili Sanifu tunasema, “**M**toto **m**zuri **a**nalia” na ‘**W**atoto **w**azuri **w**analia’ katika hali ya umoja na wingi mtawalia. Katika Kiolusuba sentensi hiyo ya kwanza ni “**O**mwana **o**mulootu **a**rra” ‘Hali ya wingi ya sentensi hiyo ni, ‘**A**waana **a**walootu **w**arra’. Katika lugha hizi mbili, tunaona viambishi {mu –} na {wa-} katika vivumishi na vitenzi vikidhihirisha upatanifu wa kisarufi. Kwa hivyo tunaweza kusema kuwa lugha ya Kiolusuba na ya Kiswahili zina asili moja na kwamba zina sifa za upatanifu wa kisarufi zinazofanana. Hata hivyo, lugha hizi zina

baadhi ya tofauti zinazojitokeza katika viwango vyote vya kiisimu kuanzia fonolojia, mofolojia na sintaksia. Tofauti hizi ni kama vile miundo ya maneno kwa mfano, katika Kiolusuba unaweza kupata mkururo wa vokali katika neno, hali ambayo si ya kawaida katika Kiswahili Sanifu. Kwa mfano maneno kama : [wa:e] na [ja:e] kumaanisha ‘wake’ na ‘yake’ mtawalia.

Nchini Kenya, Kiswahili Sanifu ni lugha inayozungumzwa na watu wengi na hata hutumika katika nyanja mbalimbali. Mawazo haya yameungwa mkono na Bakari (1982) anayeeleza kwamba Kiswahili ndiyo lugha ya Kiafrika inayozungumzwa na watu wengi zaidi ya zote katika Afrika ya Kati na Mashariki. Iribemwangi na Mukhwana (2011) na Okombo (2001) wameitaja kama *Lingua Franca* inayozungumzwa katika maeneo ya Kusini mwa Sahara barani Afrika.

Kiswahili ni lugha yenye majukumu mengi nchini kenya. Imekuwa ikitumika kwa miaka takriban hamsini kama lugha ya taifa. Hata hivyo, hivi sasa imepandishwa hadhi kupitia katiba ya Kenya ya mwaka wa 2010 na kufanywa kuwa lugha rasmi. Kwa sababu hii, Kiswahili hutumika katika shughuli rasmi kama vile bungeni, shughuli za elimu na biashara. Aidha Kiswahili ni somo la lazima katika shule za msingi na za sekondari za serikali.

1.2 Tatizo la utafiti

Kazi za wataalam mbalimbali zimeonyesha kwamba aghalabu kuna athari za Lugha ya kwanza (L_1) katika matumizi ya lugha ya pili (L_2). Corder (1967) akizungumzia mwingiliano wa lugha na mapokezi ya lugha ya pili, anasema kuwa makosa katika lugha ya pili yanaonyesha hali fulani ya matatizo aliyo nayo mzungumzaji katika L_2 kutokana na kuhamisha sifa fulani za L_1 hadi kwenye L_2 . Kazi ya Onyango (1997), Ndung’u (1999) na Mutugu (2001) ni mifano inayoonyesha kuwa watumizi wengi wa Kiswahili kama L_2 hukumbwa na matatizo katika matumizi yake kama L_2 . Makosa hayo hujitokeza katika viwango vya kifonolojia, mofolojia na hata sintaksia.

Wazungumzaji wa asili ya Kiolusuba ambao pia hutumia Kiswahili Sanifu kama lugha yao ya pili nao huathiriwa na sauti za lugha yao katika matumizi ya Kiswahili. Athari hiyo hujitokeza katika viwango vyote tulivyotaja hapo awali. Aidha hudhihirika katika matamshi na maandishi hasa katika kazi zilizoandikwa na wanafunzi kama vile insha.

Aidha matokeo ya wanafunzi katika mitihani ya kitaifa katika somo la Kiswahili huwa duni. Tukiangazia kwa mfano matokeo ya mitihani ya miaka ya 2010, 2011 na 2012 kulingana na ripoti rasmi ya Baraza La Mitihani ya Kitaifa ya Kenya, asili mia sabini ya wanafunzi waliofanya mitihani ya kitaifa hawakufikisha hata asili mia hamsini kwenye somo la Kiswahili. Kiwango hiki ni chini ya wastani. Baadhi ya makosa ya kifonolojia ni yale ya kudondoa sauti zisizopatikana katika Kiolusuba kama /h/ kwa mfano wanatamka na kuandika /akuna/ badala ya [hakuna]. Wakati mwingine wanapachika sauti hiyo pasipostahili kwa mfano /hamka/ badala ya [amka]. Pia wanatumia sauti zilizopo katika Kiolusuba kuchukua nafasi ya sauti zisizokuwepo ambazo wana matatizo ya kuzitamka, kwa mfano /s/ badala ya /ʃ/ kwa hivyo wanasema /sika/ badala ya [ʃika].

Aidha, athari nyingine hudhihirika katika miundo ya maneno isiyo sahihi. Kwa mfano, maneno yanayohusisha kudondoshwa kwa fonimu kama vile /u/ katika neno [mgeni] yanaandikwa kama /mugeni/ badala ya [mgeni]; /mulogi/ badala ya [mlogi].

Hatuwezi kupuuza kiwango cha mofolojia kwani vipengele muhimu vya utafiti huu pia hujitokeza kwenye mofu muhimu za ngeli tofautitofauti husika. Miundo ya maneno kwa ujumla inastahili kuchunguzwa. Kwa mfano vimilikishi katika ngeli ya saba ambavyo mofu zake za viambishi ni {ki-} na {tʃ-} huhusisha ukaakaishaji katika Kiswahili Sanifu lakini mfanyiko huu haupo katika Kiolusuba. Kwa hivyo wazungumzaji wa Kiolusuba aghalabu huhamisha kanuni za lugha yao katika matumizi ya Kiswahili Sanifu. Kwa mfano, wanasema /j+anɣu/ badala ya [tʃanɣu] au /j+ aŋe/ badala ya [tʃaŋe].

Corder (1971) anaeleza kuwa kila lugha ina muundo wake na kuhamisha sauti fulani au mpangilio wa L₁ katika L₂ hudhihirika kama makosa. Kutokana na mifano tuliyotoa hapo juu, ni dhahiri kwamba kuna athari za sauti za Kiolusuba katika matumizi ya Kiswahili miongoni mwa wazungumzaji wa Kiolusuba kutokana na tofauti kati ya lugha hizo. Hali hii ndiyo ilitupa msukumo wa uchunguzi ambapo tumezibainisha fonimu za Kiolusuba na kuzilinganisha na za Kiswahili Sanifu ili kuthibitisha iwapo kuna tofauti kubwa kati ya fonimu hizo na iwapo tofauti hizo ndizo zinasababisha matatizo hayo katika matumizi ya Kiswahili Sanifu. Aidha, tumechunguza miundo ya

silabi za lugha hizi na kuchunguza iwapo tofauti baina yake huchangia katika athari hiyo.

Katika utafiti huu, tumechunguza mifanyiko ya kifonolojia kati ya Kiolusuba na Kiswahili Sanifu na ikiwa tofauti hizo zinaweza kuzua matatizo katika matumizi ya Kiswahili Sanifu. Kwa ujumla, tumeyainisha na kueleza matatizo yanayotokana na tofauti za kisauti yanayojitokeza katika matumizi ya Kiswahili Sanifu miongoni mwa wazungumzaji wa Kiolusuba na kueleza visababishi vya athari kwani kuvitambua visababishi hivyo ni hatua muhimu katika harakati za kurekebisha na kukitumia Kiswahili Sanifu kwa ufasaha.

1.3 Madhumuni ya utafiti

Utafiti huu ulinua kutekeleza yafuatayo:

1. Kubainisha fonimu za Kiolusuba zikilinganishwa na za Kiswahili Sanifu.
2. Kueleza tofauti za miundo ya silabi katika Kiolusuba na Kiswahili Sanifu.
3. Kuonyesha jinsi tofauti katika mifanyiko ya kifonolojia kati ya Kiolusuba na Kiswahili Sanifu inavyochangia katika kuathiri matumizi ya Kiswahili miongoni mwa wazungumzaji wa Kiolusuba.
4. Kueleza athari za Kiolusuba katika matumizi ya Kiswahili Sanifu zinazodhihirika kimatamshi na katika kazi andishi za wanafunzi wanaozungumza Kiolusuba kama L_1 .

1.4 Nadharia tete

Baadhi ya majibu tuliyotarajia kutokana na utafiti huu ni:

1. Fonimu za Kiswahili Sanifu zisizopatikana katika Kiolusuba huwatatiza wazungumzaji wengi wa Kiolusuba kama L_1 katika matumizi ya Kiswahili.
2. Miundo ya maneno katika Kiolusuba ni tofauti na miundo ya maneno katika Kiswahili Sanifu.
3. Tofauti kati ya mifanyiko ya kifonolojia baina ya Kiolusuba na Kiswahili Sanifu huathiri matumizi ya Kiswahili.
4. Kuna maneno mengi yanayodhihirisha athari za kimatamshi katika mazungumzo na kazi andishi za wanafunzi wenye asili ya Kiolusuba katika matumizi ya Kiswahili Sanifu.

1.5 Sababu za Kuchagua Mada Hii

Pana haja ya kushughulikia athari za kimofonolojia zinazotokana na athari za L_1 (Kiolusuba) katika L_2 (Kiswahili) kwa kuwa uchunguzi wa athari hizo utasaidia katika harakati za kujaribu kuyarekebisha makosa ya kimatamshi miongoni mwa wanafunzi. Kama anavyosema Corder katika kazi ya Kinsella (1971), makosa yanayotokana na athari za L_1 katika L_2 yanaweza kutabirika kwa kuchunguza miundo ya maneno baina ya lugha ya kwanza na lugha pokezi (L_2). Matokeo ya uchunguzi huu yatakuwa ya manufaa kwa walimu ambao wataweza kuyarejelea ili kutabiri uwezekano wa kutokea kwa makosa hayo katika matumizi ya Kiswahili Sanifu miongoni mwa wanafunzi wanaozungumza Kiolusuba. Kwa hivyo, wataweza kuzishughulikia athari kama zile tulizotaja hapo awali kwa njia mwafaka. Zaidi ya hayo, inahofiwa kwamba lugha ya Kibasuba inafifia na huenda ikafa. Utafiti huu unaweza kuizindua serikali ili iweze kuweka mikakati ya kuihifadhi lugha hii kama vile kuiratibisha miongoni mwa masomo ya lazima katika madarasa ya chini katika maeneo ambamo lugha hii hutumika kama L_1 . Aidha Kiswahili ni lugha iliyo na majukumu mengi kama tulivyoeleza awali. Zaidi ya kuwa ni lugha inayotumiwa katika mawanda mapana kama vile siasa, utawala na biashara miongoni mwa mengine, pia ni lugha inayowaunganisha wanajamii mbalimbali kwa kuwa hutumiwa na wazungumzaji ambao lugha zao za kwanza ni tofauti. Pia Kiswahili ni mojawapo kati ya masomo ambayo hutahiniwa katika mitihani ya kitaifa. Utafiti huu pia utakuwa na mchango katika kusesitiza nafasi ya Kiswahili kama lugha rasmi na ya taifa. Ikumbukwe kuwa ni lugha yenye kanuni zake zinazostahili kuzingatiwa katika matumizi yake ya kila siku.

1.6 Upeo na mipaka

Kazi hii imeangazia athari zinazodhihirika katika matumizi ya Kiswahili miongoni mwa watu ambao lugha yao ya kwanza ni Kiolusuba. Wanaisimu kama vile Nickel (1972) katika Lange (1974) na Corder (1973) wanakubaliana kwamba makosa ya L_1 kwa L_2 yanatokea katika viwango vyote vya lugha yaani fonolojia, mofolojia na hata sintaksia. Mawazo haya yameungwa mkono na Valdman (1975) aliyeorodhesha data ya lugha 246 zilizo na athari za L_1 kwa L_2 katika sintaksia, matamshi, tahajia na hata katika msamiati.

Utafiti huu hata hivyo, haukushughulikia viwango hivyo vyote vya lugha kwa ukosefu wa muda. Kwa hivyo, tumeshughulikia kiwango cha fonolojia na mofolojia. Katika kutoa maelezo ya kina, tumelazimika kutumia elementi fulani za kisintaksia tukiwa na lengo la kueleza maswala ya kisauti katika matumizi ya lugha ya Kiolusuba na Kiswahili. Tumeshughulikia maswala ya kiwakati lakini mara kwa mara tumeweza kurejelea maswala ya kimapisi ilipohitajika.

1.7 Yaliyoandikwa kuhusu somo hili

Ingawa mengi yameandikwa kuhusu jinsi lugha nyingi zinavyoathiri Kiswahili Sanifu, ikumbukwe kuwa kila lugha ina muundo na sifa zake, kwa hivyo kila lugha huathiri Kiswahili kwa njia yake ya kipekee. Zaidi ya hayo, yaliyoandikwa pia hutofautiana. Kwa kuwa tumeshughulikia athari hizo kwa kuzingatia mofofonolojia ya Kiolusuba, tulirejelea yaliyoandikwa kuhusu: athari za L_1 kwa L_2 , fonolojia na mofolojia na ulinganishi wa mofofonolojia za lugha mbalimbali na Kiswahili Sanifu.

1.7.1 Yaliyoandikwa kuhusu athari za L_1 kwa L_2

Kazi ya Corder (1967) inaeleza kuwa matatizo yanayojitokeza mtu anapojifunza L_1 na L_2 ni jambo la kawaida kutokea kabla ya mtumizi lugha kuzoea matumizi kamili ya kanuni za lugha ya pili. Anaeleza kwamba, kuna tofauti kati ya makosa na matatizo. Kwake Corder, makosa ni matatizo yanayotokana na utendaji na hayana ruwaza yoyote na yanaweza kutokea kwa hali zozote. Aidha, kulingana naye Corder makosa hayana uzito kama vile matatizo kwa sababu matatizo yanadhihirika kwa kuzingatia umilisi wa lugha.

Kutokana na kazi ya Selinker (1969), tunapata kuwa kuna mifanyiko mitano ya kisaikolojia ambayo ni muhimu katika kuchanganua matatizo katika matumizi ya lugha. Mifanyiko hiyo ni pamoja na: ujumlishaji mno kutokana na mifumo ya L_2 inayotumiwa kiholela, uhamishaji lugha ambapo kanuni za L_1 hutumiwa na hivyo kukiuka kanuni za L_2 , mikakati ya mawasiliano katika L_2 , njia za kujifunza zisizokuwa halisi, na uhamishaji wa ufundishaji ambapo makosa hutokana na kutokuwa na umilisi kwa wanaofundisha. Kila aina ya tatizo hudhihirika katika njia hizo alizotaja Selinker. Kulingana na Selinker, makosa hayo yanaibua kiwango kingine katika matumizi lugha kinachoitwa lugha-kati. Lugha kati ni lugha inayojitokeza wakati ambapo

mzungumzaji yuko katika harakati za kujifunza L_2 . Mzungumzaji wa lugha kati huhamisha kanuni za L_1 kwa lugha lengwa. Kazi hii ya Selinker ilichangia katika kazi yetu kwa kuwa ilituwezesha kuyaainisha makosa kutumia baadhi ya vigezo alivyovitaja. Hata hivyo ikumbukwe kwamba Selinker alishughulikia lugha kwa jumla kwa kurejelea vipengele mbalimbali. Kwetu sisi tuliangazia athari za kisauti za lugha mahususi L_1 (Kiolusuba) kwa L_2 (Kiswahili).

Aidha, Selinker (1972) anaeleza kwamba mfumo huu mpya unaojitokeza unaweza kuchunguzwa kwa kushirikisha wanaojifunza L_2 katika maandishi na mazungumzo. Selinker aligundua kwamba kadri wanafunzi wanavyozidi kujifunza ndivyo matatizo ya matumizi lugha yanavyozidi kudidimia. Jambo hili tulitazamia kulithibitisha katika sampuli yetu iliyokuwa na wanafunzi wenye umilisi ulio sawa katika matumizi ya Kiolusuba kwani wote ni wazawa wake bali wana umilisi tofauti katika Kiswahili kulingana na madarasa yao shuleni. Wanafunzi katika madarasa ya juu wana umilisi wa juu katika Kiswahili kuliko wale walio katika madarasa ya chini kwa kuwa muda ambao wameutumia katika mawasiliano na kufundishwa Kiswahili ni tofauti.

Chepkwony (1993) alichunguza makosa ya kifonolojia miongoni mwa Wanandi katika matumizi ya Kiswahili. Hakushughulikia mofofonolojia na kwa hivyo hakujishughulisha na miundo ndani na miundo nje ya maneno na jinsi inavyochangia katika athari hii. Zaidi ya hayo alishughulikia lugha mbili zilizo na sifa tofauti kabisa kwani Kinandi ni lugha ya Kinailoti ilhali Kiswahili ni Kibantu. Aidha, Kazi yetu ilishughulikia viwango viwili vya fonolojia na mofolojia.

Were (1994) alitafiti kuhusu athari zinazotokana na L_1 zinazodhihirika katika uandishi wa insha za Kiswahili. Yeye alishughulikia makosa ya kimsamiati, tahajia na pia sarufi. Katika utafiti wake, Were alitambua kwamba kuna ile hali ya wanafunzi kujumlisha sheria na pia kuzihamisha kutoka L_1 hadi L_2 ambayo ni Kiswahili Sanifu. Hata kama ulinganifu upo, utafiti wake haukufanywa kwa kulinganisha athari za lugha ya Kiolusuba kwa Kiswahili Sanifu.

Onyango (1997) alichunguza iwapo tofauti za kisarufi za Kinyala na Kiswahili ni kikwazo katika matumizi ya Kiswahili. Uchunguzi huu haukujikita kwa undani hasa kuchunguza elementi za kisauti na miundo ya maneno. Ulijikita sana katika upatanifu

wa kisarufi ambao ni mwelekeo wa kisintaksia bila kuhusika na matamshi. Kazi yetu ilizingatia jinsi sauti za Kiolusuba zinavyoathiri matumizi ya Kiswahili Sanifu.

Mutugu (2001) alichunguza makosa ya kileksia yanayofanywa na wanafunzi wa kidato cha pili katika insha zao. Hata ingawa kazi hii yaelekea kuwa karibu na yetu, makosa ya kileksia hujumlisha makosa ya tahajia na hata msamiati ambao kwetu si muhimu. Huenda hayo yakashughulikiwa kwa kiwango kingine. Kazi ya Mutugu ilihusika tu na miundo nje ya maneno.

Rapando (2005) alihusika na kuchunguza makosa ya kimofosintaksia miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili katika uandishi wa insha jijini Nairobi. Alishughulikia wanafunzi walio na asili anuwai ambao huenda hawana makosa ya sampuli ya kutabirika kwa kuwa baadhi ya makosa aliyoyashughulikia yanatokana na Kiingereza na 'Sheng' ambayo ni lugha kipindi inayobadilika kila mara. Aidha baadhi yao wanaathirika na L₁ ya wazazi wao. Kazi yetu ni tofauti kwani ililenga kundi mahususi ambalo lingeweza kuchunguzwa na matokeo ya kijumla kufikiwa. Pia tuliwahasisha wanafunzi wa shule za msingi walio na umilisi wa Kiswahili Sanifu usio sawa kulingana na madarasa husika.

1.7.2 Yaliyoandikwa kuhusu mofofonolojia za lugha nyingine zikilinganishwa na Kiswahili

Kazi nyingine ambazo zimetusaidia ni zile zilizoshughulikia mofofonolojia za lugha mbalimbali za Kibantu tofauti na Kiswahili. Kazi hizo ni pamoja na Bakari (1982) ambaye alichunguza mofofonolojia ya lahaja za Kiswahili na Mukuria (1987) ambaye alilinganisha ngeli za Kiswahili Sanifu na Kikikuyu cha Kabete. Hata ingawa kazi yetu inasheheni mambo kadhaa yanayofanana na kazi hizi kama vile ngeli na mifanyiko ya kifonolojia, kazi yetu inatuelekeza katika kueleza chanzo cha makosa katika matumizi ya Kiswahili. Aidha inatuelekeza katika kubashiri uwezekano wa makosa kutokea katika mazingira fulani ya matumizi ya Kiswahili Sanifu.

1.7.3 Yaliyoandikwa kuhusu fonolojia na mofolojia za lugha mbalimbali

Polome (1967) ametalii sana maswala ya fonolojia, mofolojia na sintaksia ya Kiswahili Sanifu pamoja na ngeli nomino zake. Maelezo yake yalikuwa na manufaa kwetu sana katika kulinganisha baadhi ya mambo ya kimofofonolojia ya Kiswahili Sanifu na Kiolusuba. Pia ameshughulikia mengi kuhusu fonetiki, ala za matamshi

pamoja na uainishaji wa fonimu. Kazi hii ilitupa mwongozo katika kushughulikia dhana ya fonimu.

Kazi ya Schane (1973) ilitusaidia sana kuelewa Nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia kwa undani kwa kuwa ni nadharia ambayo ilitokana na Nadharia ya Fonolojia Zalishi ambayo ametailii kwa kina. Ameshughulikia swala la sheria na kuziainisha katika makundi matatu makuu. Makundi yenyewe ni:

- ❖ Kanuni za usilimisho
- ❖ Kanuni za muundo mwafaka wa silabi, na
- ❖ Kanuni za kutofautiana kisifa kadri inavyowezekana

Schane anasisitiza kwamba kanuni au sheria asilia ndizo zile zinazopatikana katika takriban lugha zote za ulimwenguni. Sheria hizo ndizo zinazotumika kuonyesha mifanyiko ya kifonolojia katika lugha asilia.

Utafiti huu ulifaidika pia na kazi ya Meinhof (1973) ambaye alichunguza fonolojia za lugha mbali mbali za Kibantu. Ameeleza mfumo mzima wa Mame Bantu ambao umeipa kazi hii mwelekeo kuhusu mabadiliko ya maneno katika Kiswahili na Kiolusuba yakilinganishwa na maneno katika Mame Bantu.

Lass (1984) ameeleza mifumo ya kifonolojia, mifanyiko ya kifonolojia, ala za matamshi na sifa bainifu za fonimu mbalimbali. Pia Iribemwangi (2010) ametoa sifa bainifu za fonimu, miundo ya maneno pamoja na mifanyiko ya kifonolojia katika Kiswahili Sanifu. Aidha ameeleza maswala yanayohusiana na Mame Bantu. Kazi hizi zote zimekuwa kama mwongozo katika kazi yetu maadamu tumeshughulikia mofofonolojia ya Kiswahili na Kiolusuba.

1.8 Msingi wa nadharia

Nadharia ambayo tumeitumia katika kazi hii kama mwongozo wetu ni Nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia (NFZA). Nadharia hii ilizuka ili kujaribu kutatua matatizo yaliyotokana na udhaifu wa Fonolojia Zalishi (FZ) uliodhihirika katika kazi za Chomsky za miaka ya 1950. Zaidi ya hayo, katika mwaka wa 1968 Chomsky na Halle walitoa kazi nyingine iliyoitwa *Sound patterns of English* (SPE) ambayo ilichunguzwa na wanaisimu kama Vennemann na kupatikana kuwa na udhahania mwingi katika uwasilishaji wa elementi zake. Hii ni kwa sababu ilisisitiza ubia katika: FZ za lugha,

sheria za Fonolojia na mpango wa ishara na vokali. Aidha, ilisisitiza kuwa uwasilishaji mlalo wa sheria ulikuwa wa lazima. Kwa ujumla nadharia hii ilishikilia kuwa lugha zote zilikuwa na sifa bia.

Venneman aliasisi NFZA katika kujaribu kutoa udhahania ulioonekana katika FZ. Hata hivyo, Joan Hooper (1971) ndiye alieleza na kuendeleza NFZA katika tasnifu yake iliyoitwa *Aspects of Generative Phonology*. Baadaye kazi hii ilychapishwa katika mwaka wa 1976 kwa kichwa cha *Introduction to Natural Generative Phonology (NGP)*. Hooper (1976), anaeleza kwamba NFZA ina uwezo wa kuonyesha umilisi wa mzawa wa lugha. Anaeleza ya kwamba sarufi huwasilisha uwezo na umilisi alio nao mzawa wa lugha unaomwezesha kutoa matamshi yasiyo na kikomo (1976:3). Anaeleza zaidi kwamba katika Fonolojia Zalishi, umilisi wa lugha unaonyeshwa kupitia sheria zinazozingatia maana za sauti zinazotumika katika lugha. Hata hivyo, aligundua kuwa nadharia ya FZ haingetupiliwa mbali tu. Hii ni kwa sababu NFZA ilikuwa na uwezo mkubwa kuliko kueleza maswala ya lugha asilia. Alisema lengo la wananadharia wa isimu ni kuvumbua nadharia iliyo na uwezo wa kueleza maswala kuhusu lugha asilia lakini sio kuwa na nguvu zaidi kiasi cha kueleza au kutabiri matukio ambayo hayapatikani katika lugha asilia (1976:4-5). Lengo kuu la Hooper lilikuwa kuasisi nadharia iliyoweza kurekebisha udhaifu wa nadharia za awali kama vile Nadharia ya Geuza Maumbo Zalishi (NGMZ) iliyotumika katika SPE ambayo ilionyesha kuwa na nguvu kuliko kutumika katika lugha asilia.

Kwa sababu Hooper anajaribu kuyatatua matatizo ya udhahania katika FZ, anaeleza kwamba ni muhimu kutambua nadharia inayokabiliana na udhaifu wake kisha kutathmini matokeo ya nadharia hiyo mpya (1976:5). NFZA huchunguza maumbo ndani ya maneno ili kupunguza udhahania. Kwa hivyo, nadharia hii ina uwezo wa kuonyesha muundo ndani wa neno kutoka kwa muundo wa nje. Hii ina maana kwamba miundo ndani ya meneno hayo inatarajiwa na kwa hivyo inastahili kuonekana katika miundo nje ili iweze kukubalika kama muundo ndani sahihi. NFZA kwa hivyo humwezesha mchunguzi wa lugha kufikia utabiri sahihi kuhusu lugha asilia. Hooper anaita jambo hili **kanuni ya ujumlishaji sahihi**. Kanuni hii inawasilisha uhusiano kati ya miundo nje na kauli za kijumla ambazo lazima zidhihirike kama ya kweli katika kila neno husika. Hooper anaeleza kwamba kanuni ya ujumlishaji sahihi inaeleza

kuwa sheria zinazowekwa na wazungumzaji wa lugha hutokana na miundo nje ya maneno bali sio miundo ndani (1976:13). Kanuni hii hairuhusu kurejelea kuwepo kwa sheria inayorejelea kipande kisichokuwepo. Sheria hii inathibiti matumizi ya ‘uwezekano’. Kwa hivyo huthibiti udhahania. Kulingana na Vennemann sheria za NGP zinaweza kutokea zaidi ya mara moja katika maneno bila kulazimisha mfuatano wa elementi zinazohusika. Venneman anasema sheria zote zinafuata ruwaza maalum katika umbo lolote linaloafikiana na muundo wa maumbo.

NFZA inajaribu kutoa udhahania kwa kupendekeza ya kwamba miundo ya ndani na nje yote iwe na uhusiano wa moja kwa moja. Hii inaitwa **kanuni ya uasilia kamili**. Katika sheria hii, vipashio vya kifonolojia vinavyojitokeza katika uwasilishaji wa kileksia wa mofimu ni zile zinazojitokeza katika muundo nje wa mofimu hiyo. Sheria hii inasisitiza kwamba kila kanuni ya sarufi ya Fonolojia yaani sheria zinazopata motisha kifonolojia na kimofolojia lazima zionyeshe ujumlishaji sahihi kuhusu muundo nje wa maneno.

Kanuni hii inaeleza ya kwamba mtu anayechunguza lugha kwa kutumia data tu ya miundo nje ya maneno hawezi kushughulikia miundo dhahania na hata hawezi kuunda sheria zilizo na ubuye.

NFZA ina makundi manne makuu ya sheria. Makundi hayo ni:

- i) Sheria za Kifonetiki
- ii) Sheria za Kimofolojia
- iii) Sheria za Via
- iv) Sheria za Sandhi.

1.8.1 Sheria za Kifonetiki

Kanuni hizi zinatokea katika mazingira ambayo ni ya kifonetiki kamilifu. Zinarejelea maumbo ya kifonetiki na mipaka ya silabi. Kanuni hizi zinahimili habari za kifonetiki tu kama vile sheria za kutamka maneno. Kwa mfano zinaeleza ni wapi kunapaswa kuwa na mghuno katika matamshi. Mfano mmoja ni ule wa sauti /s/ ya hali ya wingi katika Kiingereza. Katika maneno fulani sauti hiyo inapata mghuno ilhali wakati mwingine hukosa mghuno. Kwa mfano katika maneno kama *pots*, *chicks*, sauti /s/ hutokea bila mghuno kwa sababu ya ujirani wake na sauti zisizokuwa ghuna. Katika

maneno kama *dogs* na *mangoes* sauti /s/ hutokea kama /z/ kimatamshi kwa sababu hupokea mghuno kutokana na kuwa katika mazingira ya ujirani na sauti ghuna. Mabadiliko ya sauti hizi hupata motisha kifonetiki ikiwa motisha hiyo huonekana kwenye muundo nje. Kanuni za ‘P’ hueleza jinsi muundo nje utajitokeza katika mazingira ya kifonetiki. Kwa mfano katika ukaakaishaji, sauti /k/ →/tʃ/[i] yaani [+nyuma] →[-nyuma]/- [-nyuma].

1.8.2 Sheria za Mofolojia ‘Mp’

Kanuni hizi zinabadilisha miundo ya maneno katika mazingira ya mofosintaksia na leksia. Kwa hivyo kanuni hizi zinaweza kurejelea kategoria za kisintaksia kama njeo, hali ya wingi wa maneno, nomino, vitenzi au maneno dhahania. Kanuni za ‘Mp’ hubeba habari za kimofolojia pamoja na za sintaksia. Tofauti kati ya sheria za ‘P’ na za ‘Mp’ ni kwamba ‘Mp’ hufungana na lugha mahususi. Kanuni hizi zinahusiana na maana katika lugha husika. Kwa mfano, jinsi mofimu fulani hutumika kuonyesha hali ya wingi. Kila lugha ina njia yake ya kipekee inayotumia kueleza mabadiliko katika mazingira ya kifonetiki. Mathalani, katika Kiswahili hali ya wingi na njeo huonyeshwa kwa njia mbalimbali kwa kutegemea ngeli ya neno kama vile:

- Mtoto mzuri alikuja – Watoto wazuri walikuja
- Kisu chepesi kinakata – Visu vyepesi vinakata

Matumizi haya ya mofu {wa-},{tʃ-} hutokea katika Kiswahili kwa upekee kwani hazidhihiriki vivyo hivyo katika lugha nyingine.

1.8.3 Kanuni za Via

Kanuni za Via zinawawezesha watu kuhusisha elementi za kileksika ambazo hutofautiana kwenye miundo nje. Kanuni hizi aghalabu hazizalishi elementi. Kwa hivyo kanuni fulani hazilinganishwi na nyingine katika maneno kwa wazungumzaji lugha. Mfano mzuri hupatikana katika maneno fulani ya Kiingereza kama vile: *go – went, stink – stench, breech – break*.

Kwa ujumla, nadharia ya FZA inajaribu kutatua suala la udhahania katika uwasilishaji wa elementi za ishara na sheria zake kwa kutambua daraja la mofolojia ambalo lilipuuzwa na FZ. Inasaidia kuonyesha mabadiliko ya kifonolojia na pia kuyaeleza kutumia kanuni mbalimbali. Nadharia hii hudhihirisha upekee wa kila lugha na kwa

hivyo ni muhimu katika kuyaweka wazi matatizo yanayoibuka katika kule kutokea kwa lugha ambayo Selinker (1960, 1972) anaitaja kama lugha kati ambayo ni lugha inayojitokeza kati ya L_1 na L_2 . Dhana hii ilitokea kwa maana ya kwamba lugha hiyo hupata sifa zake kutoka kwa lugha zote mbili. Hata hivyo, ikumbukwe kuwa lugha huwa ni mali ya jamii kama anavyodai Cook (1969:12) katika Habwe na Karanja (2004). Kila lugha huwa na sifa zake na kanuni zisizoweza kubadilishwa ili kutosheleza lugha nyingine. Kwa hivyo, katika kuchunguza sauti na mabadiliko yake katika Kiswahili na Kiolusuba, tumeangazia zaidi matatizo yaliyopo miongoni mwa wazungumzaji wa lugha hizi mbili, Kiolusuba ikiwa L_1 na Kiswahili ikiwa L_2 kwao kimatumizi.

1.8.4 Sheria za Sandhi

Sheria hizi hazina habari nyingine zisizo za kifonolija bali huonyesha mipaka katika miundo ya maneno. Zinahusisha kundi maalum kati ya sheria za '*P*' na sheria za '*Mp*'. Hii ni kwa sababu mipaka ya maneno katika kanuni za sandhi lazima zichukuliwe kama mipaka ya sintaksia kwa sababu inapambanuliwa na sintaksia na semantiki wala sio fonolojia. Kwa upande mwingine mpaka wa neno hufanana na mpaka wa kifonolojia kwani wakati mwingine mpaka wa neno hutokea kisadfa pamoja na mpaka wa silabi yaani mwanzo na mwisho wa silabi. Mipaka hiyo inapotokea hivyo, hutokea kama sheria ya kifonetiki. Lass (1984) anasema kuwa mfano wa sheria ya Sandhi hutokea wakati ambapo vokali zinazofanana huvutana na kutokea kama sauti nyingine. Kwa mfano; /*wa+ingi*/ → [*wɛŋgi*].

1.9 Njia za utafiti

1.9.1 Utangulizi

Ili kufikia malengo ya utafiti kwa njia mwafaka katika mipaka ya nadharia husika, harakati za utafiti lazima zishughulikiwe kwa utaratibu. Kent (1978) anasema kuwa utafiti ni njia taratibu ya kufikia ujuzi na maarifa. Kazi hii ni ya utafiti fafanuzi kwani ni kazi inayochunguza data na kueleza jinsi ilivyo. Nadharia ya FZA imekuwa muhimu kwetu kwani ndiyo imetumika kueleza kwa kina miundo halisi ya maneno na kwa hivyo kuangazia athari za Kiolusuba katika matumizi ya Kiswahili. Aidha nadharia hii ya FZA hutumika kueleza maswala ya lugha asilia kama vile Kiolusuba.

1.9.2 Uteuzi wa sampuli

Kiolusuba kama mojawapo kati ya lahaja zinazozungumzwa na Wabasuba huzungumzwa kwenye kisiwa cha Mfangano. Hata hivyo si sehemu zote za Mfangano ambapo wazungumzaji asilia wa Kiolusuba wanaishi. Lahaja hii inazungumzwa katika sehemu za Magharibi mwa Mfangano. Tumetumia sampuli ya nasibu ya watoto thelathini miongoni mwa wazungumzaji wa Kiolusuba. Kwa hivyo, sampuli yetu tuliipata kutoka kwa shule za msingi mbili zinazopatikana katika sehemu hiyo. Kuna shule nyingine kule lakini shule tulizozitumia ni Uozi na Wakinga. Sababu yetu ya kuchagua shule hizi ni kwamba zinapatikana katikati mwa eneo ambapo lugha ya Kiolusuba huzungumzwa na watoto karibu wote huitumia kama L_1 nyumbani.

1.9.3 Mbinu za ukusanyaji data

Tulitumia data msingi na data za maktabani. Data msingi ni ile tuliipata kutoka kwa wazungumzaji wenye asili ya Kiolusuba nyanjani. Zaidi ya hayo tulitumia ujuzi wetu wa lugha hii. Baadhi ya maneno tuliyoyachunguza tuliipata katika *Endagano Empia* Biblia ya Kiolusuba. Pia tuliwahoji wazungumzaji asili wa Kiolusuba kuhusu baadhi ya maneno. Zaidi ya hayo tulikitembelea kituo cha utangazaji cha redio cha *Ekialo Kiona* ambapo tulipata data kutoka kwa watangazaji wanaotumia Kiolusuba katika kusambaza habari. Tulivyotaja hapo awali, tulinuia kutumia sampuli ya nasibu ya wanafunzi thelathini katika shule mbili za msingi. Wanafunzi tuliowahusisha ni wa madarasa ya nne, sita na nane. Tuliwahusisha wanafunzi kulingana na orodha rasmi ya madarasa yao. Waliohusika ni: wa kwanza, wa saba, wa kumi na sita, wa kumi na tisa na wa ishirini na tano katika kila darasa husika. Wanafunzi hao waliandika insha ambazo tulizisahihisha kwa makini na kujaribu kuyachanganua makosa yao huku tukiyaainisha katika makundi kulingana na aina zake. Kwa mfano, athari zinazosababisha kudondosha sauti zisizopatikana katika Kiolusuba kama /h/. Pia tulinasabaadhi ya mazungumzo ya wazawa wa Kiolusuba ili kusikiliza jinsi walivyoathirika katika matumizi yao ya Kiswahili. Aidha, tuliwahusisha katika kuandika imla ili tuchunguze iwapo maneno hayo yaliyoandikwa kutokana na imla yana athari kutokana na Kiolusuba.

1.9.4 Mbinu za uchanganuzi wa data

Baada ya kutoka nyanjani, tuliyasikiliza mazungumzo tuliyoyanasa kwa makini na kuyadondoa maneno yanayoashiria athari ya Kiolusuba. Pia tuliyaaanisha makosa katika insha na imla na kuyachorea jedwali ili kuonyesha asili mia ya kutokea kwa kila aina ya kosa. Kila kitengo, yaani insha, imla na rekodi iliyonaswa ilichorewa jedwali lililoonyesha makosa yalivyojitokeza katika akisami ya wanafunzi waliohusika kisha kubadilisha takwimu hizo katika asilimia.

1.9.5 Njia za uwasilishaji wa data

Data yetu imewasilishwa kwa njia ya kuyaaanisha maneno kulingana na athari zilizodhirika kimatumizi huku tukitoa maumbo sahihi. Aidha, tumeeleza sababu za kutokea kwa kila aina ya athari. Kisha, tumewasilisha data kwa jedwali lililoonyesha asili mia na baa grafu inayotoa habari hiyo ya jedwali kwa njia ya mchoro.

1.10 Hitimisho

Katika sehemu hii, tumeeleza jinsi tulivyoyafikia malengo yetu kupitia njia za utafiti za maktabani na nyanjani. Tumeeleza kuhusu kazi yetu kwa kurejelea mambo mbalimbali kama vile tatizo la utafiti, sababu ya kuchagua mada hii, yaliyoandikwa kuhusu mada hii, madhumuni, haipotesia na msingi wa nadharia inayotuongoza. Aidha, tumeeleza jinsi tulivyoiteua sampuli yetu kule nyanjani na tulivyoikusanya data yetu. Pia, tumeshughulikia jinsi tulivyoichanganua data hiyo na hatimaye kuiwasilisha kwa kutumia jedwali na baa grafu katika maelezo.

2. SURA YA PILI

2.1 FONIMU ZA KISWAHILI SANIFU NA KIOLUSUBA

2.1.1 Utangulizi

Katika sura hii, tuliziainisha fonimu za Kiswahili Sanifu na za Kiolusuba. Ili kuelewa mifumo ya lugha hizi mbili kikamilifu, ni muhimu kuelewa mifumo ya sauti zake. Jones (1989) anasema kuwa, kuelewa mfumo wa sauti za lugha yoyote kikamilifu hakuwezekani bila kubainisha kati ya sauti za kimatamshi na fonimu. Dhana ya fonimu hushugulikiwa katika tawi la isimu la Fonolojia. Hyman (1975) anaelezea tawi hili kama mtalaa wa mfumo wa sauti yaani linashugulikia jinsi sauti hupangwa pamoja na uamili wake katika lugha mahususi. Kulingana na Jones, sauti za kimatamshi ni zile zinazotokana tu na ala za kimatamshi na pia zina sifa za kiakustika bali hazibadiliki ilhali fonimu ni kipashio kimojawapo katika kikundi maalum cha vipashio ambavyo vina uhusiano na hutumika aghalabu katika lugha husika pamoja na sauti nyingine ambazo huweza kuchukua nafasi yake katika ruwaza fulani za kisauti. Mawazo haya yanasawiana na ya Massamba na wenzake (2004). Wanaeleza kwamba fonimu ni kipashio kidogo ambacho hudhihirika kama sauti katika lugha mahususi. Wanaongezea ya kwamba uamilifu hasa wa fonimu ni kutofautisha maana ya maneno. Kwa mfano, katika Kiswahili Sanifu maneno [hama] na [hamu] yana fonimu sawa isipokua zile za mwisho [a] na [u]. Fonimu hizo ndizo zinaleta tofauti ya maana.

Iwapo sauti fulani inayopatikana katika neno fulani itaondolewa na badala yake sauti nyingine kuwekwa, sauti hiyo iliyowekwa ikibadilisha maana ya neno hilo basi sauti hizo husika ni fonimu za lugha hiyo. Kwa mfano sauti [l] na [r] katika maneno [mahari] na [mahali]. Tunapoondoa [r] na kuweka [l] maana hubadilika. Sauti hizo mbili ni fonimu za Kiswahili. Ikumbukwe kwamba iwapo sauti moja itakosa kuleta maana katika lugha fulani, sauti hiyo itakosa hadhi yake kama fonimu.

2.1.2 Fonimu za Kiswahili Sanifu

Kwa kuwa kazi hii inategemea kwa kiwango kikubwa fonimu za Kiswahili na za Kiolusuba, tutachunguza vipengele muhimu vya kipashio hiki kuhusiana na lugha hizi. Kiswahili na Kiolusuba ni lugha asilia za Kibantu. Kwa hivyo lugha hizi mbili zina

sauti nyingi zinazofanana. Hata hivyo zina tofauti pia za kisauti kwani hakuna lugha mbili ambazo hufanana kikamilifu katika mifumo ya kisauti.

Baadhi ya wanaisimu wameushughulikia mfumo wa fonimu za Kiswahili. Miongoni mwao ni Mgullu (2001), Massamba na wenzake (2004) na Iribemwangi (2010). Wote wameziainisha fonimu kama:

- i. Fonimu za irabu
- ii. Fonimu za nusu irabu
- iii. Fonimu za konsonanti

2.1.2.1 Fonimu za irabu za Kiswahili Sanifu

Kiswahili Sanifu kina irabu tano ambazo ni: /a/, /ε/, /i/, /ɔ/ na /u/ sauti hizi za irabu ndizo huungana na za konsonanti ili kuunda silabi. Sauti za irabu hutamkwa pasipo kuzuiliwa hewa popote kinywani. Irabu zinaweza kuainishawa kwa kutumia vigezo vitatu. Vigezo hivyo ni:

Sehemu ya ulimi

Hapa tunarejelea sehemu ya ulimi inayohusika wakati wa kutamka irabu. Sehemu hii inaweza kuwa ya mbele, kati au nyuma. Katika Kiswahili Sanifu irabu za mbele ni /ε/ na /i/ ilhali zile za nyuma ni /ɔ/ na /u/. Irabu ya kati ni /a/.

Mwinuko wa ulimi

Ulimi unaweza kuinuliwa juu ukawa sambama na sehemu ya juu mwa kinywa, unaweza kulazwa chini kinywani au ukawa katikati ya sehemu hizi. Irabu zitamkwazo ulimi ukiwa umeinuliwa juu na sambamba na paa la kinywa ni za [+juu] nazo ni /i/ na /u/. Irabu zinazotamkwa ulimi ukiwa katikati ni /ε/ na /ɔ/. Irabu ambayo hutamkwa katika sehemu ya chini mwa kinywa ni /a/. Irabu /ε/ na /ɔ/ zina sifa ya [-kaze] yaani zinapotamkwa ulimi hulegezwa ukilinganishwa na wakati wa kutamka /a/, /i/ na /u/ ambazo hutolewa ulimi ukiwa umekazwa. Sauti hizi huwa na sifa ya [+kaze].


Mkao wa mdomo

Mdomo unaweza kuwa na mkao wa mviringo au umetandazwa wakati wa kutamka irabu. Irabu zinazotamkwa mdomo ukiwa na mkao wa mviringo ni /ɔ/ na /u/. Wakati ambapo mdomo umetandazwa, ni irabu /a/, /ε/ na /i/ zinazotolewa. Hata hivyo

kiwango cha mvingo au kutanda huwa tofauti kulingana na irabu inayohusika mathalani mdomo hutanda wakati wa kutamka /a/ zaidi ya /ε/ na /i/.

Irabu za Kiswahili hutamkwa kama tunavyoonyesha kwenye mchoro unaofuata.

Kielelezo 2.1 Fonimu za Irabu za Kiswahili Sanifu



Kielelezo 2.2 Jedwali la irabu za Kiswahili Sanifu

	/a/	/ε/	/i/	/ɔ/	/u/
<i>Juu</i>	-	-	+	-	+
<i>Chini</i>	+	-	-	-	-
<i>Nyuma</i>	-	-	-	+	+
<i>Mbele</i>	-	+	+	-	-
<i>Mviringo</i>	-	-	-	+	+
<i>Kaze</i>	+	-	+	-	+
<i>Kati</i>	+	-	-	-	-

Katika jadwali hili tunaona ya kwamba irabu ambazo ni [+juu] na [+nyuma] zina sifa za [+mviringo]. Kwa hivyo /u/ ambayo ni sauti ya [+juu] na pia [+nyuma] ina sifa ya [+mviringo]. Vivyo hivyo sauti za [-nyuma] na [-juu] ni [-mviringo]. Sauti hizo ni /a/ na /ε/. Vile vile, sauti za [-chini] na [-nyuma] ni [+mbele] nazo ni /ε/ na /i/. Sauti za [-chini] na [-juu] ni [-kaze]. /a/ pekee ndiyo [+kati].

2.1.2.2 Fonimu za Nusu irabu za Kiswahili Sanifu

Kiswahili kina nusu irabu mbili. Nusu irabu pia huitwa viyeyusho. Hizi ni sauti za lugha zinazotamkwa kwa kuachilia hewa kutoka katika mapafu kupitia kinywani au kwenye mkondo hewa wa pua kwa mkaruzo mdogo. Fonimu za nusu irabu ni /w/ na

/j/. */w/* hutamkwa mdomo ukiwa na mkaao wa mviringo na shina la ulimi limevutwa nyuma kuelekea kwenye kaakaa laini. */j/* hutamkwa midomo ikiwa imetanda huku bapa la ulimi ukiwa umeinuliwa kuelekea kaakaa gumu. Sauti hizi kama anavyoeleza Iribemwangi (2010) zinadhihirika wazi katika mifanyiko ya kifonolojia hasa uyeyushaji.

2.1.2.3 Konsonanti za Kiswahili Sanifu


Kufikia sasa hakuna uwiano kabisa kuhusu idadi kamili ya konsonanti za Kiswahili Sanifu. Polome (1967) aliorodhesha konsonanti 24, Massamba na wenzake (2004) wameanisha konsonanti 23. Mgullu (2001) amesawiana na Polome kwani ameziorodhesha konsonanti 23 pia. Iribemwangi (2010) ameorodhesha konsonanti 25. Utafiti huu utatumia idadi hii ya ishirini na tano.

2.1.2.4 Uainishaji na sifa bainifu za konsonanti za Kiswahili Sanifu

Konsonanti za Kiswahili Sanifu ziko katika makundi sita makuu. Makundi hayo ni vipasuo, vizuiwa kwamizwa, vikwamizwa, nazali, vitambaza na vimadende.


Vipasuo /konsonanti za mtuo

Sauti hizi huitwa vizuiwa kutokana na sababu kwamba wakati wa kuzitamka, hewa huzuiliwa katika ala za matamshi na baadaye huachiliwa ghafla kiasi kwamba sauti hutoka kwa nguvu au mpasuo. Kiswahili kina vipasuo sita. Vipasuo hivyo ni: **/p/**, **/b/**, **/t/**, **/d/**, **/k/** na **/g/**.



Vizuiwa kwamizwa

Wakati wa kuzitamka sauti hizi, hewa huzuiliwa kwenye kaakaa gumu wakati ambapo ulimi huikaribia sana. Kisha hewa huachiliwa ghafla lakini mkondo hewa haufunguliwi wote na kwa sababu hiyo hewa hutoka kwa kutatizika na kusababisha mkwamzo. Sauti hizi ni mbili katika Kiswahili Sanifu. Sauti hizo ni |t| na /j/



Vikwamizwa

Katika kutamka sauti hizi, ala za matamshi tofauti tofauti kama vile meno na ulimi hukaribiana sana kiasi cha kufanya hewa kupitishwa katikati ya ala hizo kwa

kukwamizwa. Kwa hivyo sauti hutokea kwa kukwamizwa. Sauti hizi ni kumi katika Kiswahili Sanifu. Nazo ni /s/,/z/,/f/,/v/,/θ/,/ð/,/ʃ/,/x/,/ç/,/h/.




Nazali

Wakati wa kutamka sauti za nazali, hewa hufungiwa mahali mbalimbali katika bomba la sauti kisha huachiliwa kupitia kwenye chemba cha pua. Wakati huo, kimio kinashuka chini na kusababisha mkondo hewa wa puani na kuzitoe sauti hizo kwa King'ong'o. Kiswahili Sanifu kina nazali tano. Nazo ni /m/, /n/, /ɲ/, /ŋ/, /ɽ/




Kitambaza

Katika kuitamka sauti hii, ncha ya ulimi hukita kwenye ufizi na kutatiza mkondo wa hewa huku hewa ikiruhusiwa kupita kandokando mwa ulimi. Kiswahili Sanifu kina kitambaza kimoja tu /l/.



Kimadende

Kimadende hutamkwa ncha ya ulimi ikigotagota kwenye ufizi huku hewa ikiendelea kupita na kusababisha mrindimo wa ulimi. Katika Kiswahili Sanifu kuna Kimadende ni kimoja pia. Sauti ya kimadende ni /r/.



Kielelezo 2.3 Jedwali la Konsonanti za Kiswahili Sanifu

	Midomo	Midomo + meno	meno	Kaakaa + ufizi	ufizi	Kaakaa gumu	Kaakaa laini	glofa	jumla
vipasuo	/p/ /b/				/t//d/		/k//g/		6
Kizuiwa vikwamizwa						/t//j/			2
vikwamizwa		/f//v/	/ø//ð/	/j/	/s//z/		/x//ɣ/	/h/	10
nazali	/m/	/ŋ/			/n/	/ŋ/	/p/		5
kitambaza					/l/				1
kimadende					/r/				1
Nusu irabu	/w/					/j/			2

2.2 Fonimu za Kiolusuba

Katika lugha nyingi Kiolusuba kikiwemo, fonimu zimegawika katika makundi mawili kwa kuzingatia kigezo cha kuzuiliwa kwa hewa wakati wa kuzitamka. Ladefoged (1982) anasema kuwa fonimu huweza kutamkwa kwa kuachilia mkondo hewa mpana au kwa kuzuiliwa. Kwa hivyo kupitia njia hizi mbili tunapata irabu na konsonanti za Kiolusuba. Nusu irabu za Kiolusuba tunaziainisha pamoja na konsonanti.

2.2.1 Fonimu za irabu za Kiolusuba

Tofauti na jinsi ilivyoaminika hapo awali kwamba lugha nyingi za Kibantu huwa na irabu kati ya tano na saba, tafiti nyingi zimeonyesha kwamba lugha nyingi za Kibantu zina irabu hata zaidi ya kumi. Ogechi (2012) anapozilinganisha EkeGusii na IgiKuria anaeleza kwamba lugha hizi mbili hudhihirisha irabu kumi zikiwemo irabu tano ndefu na tano fupi. Katika juhudi za kusanifisha na kuziunganisha lugha za Kikikuyu, Kimbere na Kiembu ambazo zinakaribiana mno, Iribemwangi (2012) anaeleza kwamba lugha hizi tatu zina jumla ya irabu kumi na nne katika kila lugha. Utafiti wetu

unaonyesha kwamba Kiolusuba kina irabu kumi ambazo zinajumuisha irabu fupi na ndefu. Ikumbukwe kwamba lugha hii imeratibishwa miongoni mwa lugha zilizo na ukuruba na EkeGusii na IgiKuria.

Mifano ya maneno yanayotokana na irabu za Kiolusuba

1. /a/ [amato]	madogo
/a:/ [ama:tɔ]	mitumbi
/ɛ/ [ɛmɛsa]	umeme
/ɛ:/ [ɛmɛ:sa]	meza
/i/ [amirɛ]	maliza
/i:/ [ami:rɛ]	siku
/ɔ/ [kɔla]	fanya
/ɔ:/kɔ:la]	palilia
/u/ [tula]	toboa
/u:/ [tu:la]	bebesha

Kuna baadhi ya maneno ya asili ya Kiolusuba yaliyo na irabu ndefu. Hata hivyo, maneno yote yanayoingizwa katika Kiolusuba ambayo ni mageni hupokezwa irabu ndefu kabla ya silabi ya mwisho. Kwa mfano:-

Kiolusuba	Lugha chanzi	Neno	Maana
2. [ɛbu:ki]	Kiingereza	book	kitabu
[ɔmusala:ba]	Kiswahili	msalaba	msalaba
[eka:lu]	Kiswahili	hekalu	hekalu
[ɛkani: sa]	Kiswahili	kanisa	kanisa
[musku:li]	Kiingereza	school	shuleni


Mifano ya maneno yenye asili ya Kiolusuba yaliyo na irabu ndefu

3. [ɔmuga:ka]	kiongozi
[ami:rɛ]	siku(zaidi ya moja)
[ɔmulɔ: tu]	mzuri
[ɔkumrɛ:ta]	kumleta
[niŋgɛ: nɔ]	leo
[ntɛ:rɛkɔ]	tua
[ama: ni]	nguvu
[wai:si:zi]	rudisha

Kama tulivyoona ni kwamba katika maneno ya asili ya Kiolusuba, irabu ndefu huweza kutokea popote ilhali katika maneno mageni ni lazima zitokee zikipakana na silabi ya mwisho.


Michoro ya irabu za Kiolusuba


Irabu za Kiolusuba ni kumi. Kuna tano zilizo fupi na tano ndefu kama tunavyoonyesha hapa chini.



Kielelezo 2.4 Irabu za Kiolusuba

Sifa bainifu za irabu za Kiolusuba





Kielelezo 2.5 Matriki ya irabu za Kiolusuba

Irabu	/ a/	/a:/	/ɛ/	/ɛ:/	/i/	/i:/	/ɔ/	/ɔ:/	/u/	/u:/
Juu	-	-	-	-	+	+	-	-	+	+
Chini	+	+	-	-	-	-	-	-	-	-
Nyuma	-	-	-	-	-	-	+	+	+	+
Mbele	-	-	+	+	+	+	-	-	-	-
Mviringo	-	-	-	-	-	-	+	+	+	+
Urefu	-	+	-	+	-	+	-	+	-	+

2.2.2 Konsonanti za Kiolusuba

Hata ingawa Mattah (2000) ameorodhesha fonimu za konsonanti za Kiolusuba kuwa ni 33, utafiti huu unapata kwamba Kiolusuba kina konsonanti 32. Hii ni kwa sababu kazi hii haitambui konsonanti /r:/ kama fonimu. Sababu ya kutoitambua ni kwamba hakuna ithibati kufikia sasa kwamba kuna konsonanti ndefu katika lugha za Kibantu. Idadi hii ya fonimu ni pamoja na konsonanti zilizozalishwa awali pamoja na zile zile za mwambatano. Vipashio hivyo ni hivi: **mf, mp, mb, nd ,ng ,nj ,nk,nt,nz,ns** .

Fonimu za Kiolusuba zimegawika katika makundi mbalimbali kama vile Vipasuo, Vizuiwa kwamizwa, vikwamizwa, nazali, vitambaza, vimadende na hata nusu irabu.

Vipasuo

Kiolusuba kina konsonanti za vipasuo sita ambazo ni **/b/ /p/ /d/ /t/ /k/ /g/**. Katika kutamka sauti hizi, hewa hufungiwa kabisa katika ala za matamshi kasha huachiliwa ghafla na kutoa sauti kwa mpasuo. Mifano ya maneno yanayoundwa na fonimu za vipasuo za Kiolusuba ni:

4. /b/ -[ɔkukuba]	kupiga
/p/- [ɛmpiria]	pesa
/d/- [ɛkikdida]	uteo
/t/ - [ɔmutwɛ]	kichwa
/g/ - [gɛ:za]	nzuri
/k/- [ɔkukɔnɔ]	mkono

Kizuiwa kwamizwa

Wakati wa kutamka sauti hii, mkondo hewa huzuiliwa kisha huachiliwa taratibu huku ikitokea kwa mkwaruzo. Kiolusuba kina fonimu moja tu ya kizuiwa kwamizwa ambayo hutolewa wakati ambapo ala sogezi ya ulimi hukaribiana sana na kaakaa gumu kiasi cha kuzuia mkondo hewa kisha kuachilia huku sauti ikitoka. Mfano wa neno linaloundwa kutokana na sauti hiyo ni:

5. /j/- [jɔja]	andika
----------------	--------

Vikwamizwa

Sauti za vikwamizwa hutolewa wakati ambapo ala za matamshi hukaribiana hivi kwamba hewa hupitishwa katikati ya ala hizo na kusababisha sauti kutoka kwa mkwaruzo. Kiolusuba kina vikwamizwa vinne **/f/ /v/ /s/ /z/**. Mifano ya maneno kutokana fonimu hizi za vikwamizwa katika Kiolusuba ni:

6. / f/- [ifu]	yetu
/v/ - [ɛkianiavu]	kinyonga
/s/ - [ɛkisuusu]	sungura
/z/ -[ɔmukazi]	mke

Nazali

Kiolusuba kina fonimu za nazali tano zinazojisimamia nazo ni **/m/, /n/,/ŋ/, /ɲ/ na /ŋ/**. Pamoja na fonimu hizo, kuna fonimu za mtuo na vikwamizwa vilivyonzalishwa

awali. Fonimu hizo ni kama **mb,ng,nj** na **nd**. Kazi hii inachukulia sauti **mp, mf, nt, nz, ns**, na **nk** kuwa ni sauti ambatano. Kwa hivyo hatutashughulikia sifa zake bainifu kwa upekee. Mifano ya maneno yanayotokana na fonimu za nazali:

7. /m/ - [ɔmwami]	mfalme
/n / - [ɔmwana]	mtoto
/ɲ / - [ɛɲɔɲi]	ndege
/ŋ / - [iŋana]	neni
/ɱ / - [ɛɱvula]	mvua

Vipasuo na vikwamizwa vilivyozalishwa awali na zile ambatano:

8. /mp/ -[ɛmpanga]	jogoo
/mb/- [ɛmbɔri]	mbuzi
/mf/- [ɛmfulu]	aina ya samaki
/nd/- [rinda]	linda
/nt/- [ɛntɔwɛ]	kiti
/ɲj/- [ɲaɲjagra]	aina ya mmea
/ŋg/- [ɛŋgɔɔŋgɔɔ]	baiskeli
/nk/-[ɛnkɛmbɔ]	nyani
/ns/- [ansi]	chini
/nz/- [ɛnze]	nje

Kitambaza

Kuna kitambaza kimoja katika kiolusuba /l/. Sauti hii hutolewa wakati ulimi hugusana na ufizi kiasi kwamba mkondo hewa hupitia kandokando mwa ulimi huku sauti ikitoka kwa kufululizwa. Mfano wa neno lenye fonimu hiyo ni:

9. /l/- [ɛnzala]	njaa
------------------	------

Kimadende

Katika kutamka kimadende, hewa husukumwa kwa nguvu kiasi cha kusababisha mtetemeko kwenye ulimi na kugotagota kwenye ufizi. Kiolusuba kina kimadende kimoja tu.

10. /r/- [ɛri:sɔ]

Jicho

Nusu Irabu

Kuna fonimu mbili za nusu irabu katika Kiolusuba. Fonimu hizo ni /w/ na /j/. Fonimu hizi hutamka kwa njia tofauti. /w/ hutamkwa kwa kuviringa midomo huku shina la ulimi likivutwa kuelekea nyuma. Mkondo hewa huwa haubanwi wakati wa kutamka /w/. Sauti /j/ hutamkwa kwa midomo iliyotanda huku bapa la ulimi likiwa limeinuliwa juu kuelekea kaakaa gumu. Mifano ya maneno yaliyoundwa kutokana na sauti hizi ni.

11. /w/-[ɔluwagɔ]



ua

/j/- [ɛja:ɛ]


yake

2.2.3 Sifa bainifu za fonimu za Kiolusuba


Vipasuo




Vizuiwa vikwamizwa




Vikwamizwa




Nazali



Kitambaza



Kimadende



Nusu irabu



Kielelezo 2.6 Konsonanti za Kiolusuba

Mahali pa kutamkwa Aina Ya Fonimu	midomo	midomo +meno	meno	kaakaa +ufizi	ufizi	kaakaa gumu	Kaakaa laini	Glota	Jumla
Vipasuo	/p/ /b/				/t/ /d/		/k/ /g/		6
Vikwamizwa		/f/ /v/			/s/ /z/				4
Vizuiwa kwamizwa						/j/			1
Nazali	m	/m/			/n/	/ɲ/	/ŋ/		5
kitambaza				/l/					1
Vimadende				/r/					1
Nusu Irabu	/w/					/j/			3
									22

Kutokana na fonimu hizo tulizoziorodhesha, ni dhahiri kwamba mifumo ya fonimu za lugha hizi mbili inatofautiana kwa upeo mkubwa. Kwa mfano fonimu hizi za konsonanti za Kiswahili Sanifu hazipo katika Kiolusuba: [ʃ], [h], [θ], [ð], [ʁ],[tʃ], [x]. Vile vile, irabu ndefu za Kiolusuba hazipo katika Kiswahili Sanifu. Hata hivyo, fonimu za irabu zote za Kiswahili Sanifu zipo katika Kiolusuba.

2.3 Hitimisho

Katika sura hii tumeshughulikia fonimu za Kiswahili Sanifu na fonimu za Kiolusuba.

Aidha, tumetoa sifa bainifu za fonimu za konsonanti na za irabu za lugha hizi mbili.

Pia, tumebainisha fonimu zinazopatikana katika kila mojawapo wa lugha hizi ambazo zinatofautisha mifumo yake ya kifonimu.

3. SURA YA TATU

3.1 MUUNDO WA SILABI KATIKA KISWAHILI NA KIOLUSUBA

3.1.1 Utangulizi

Katika sura hii tunajadili tofauti za kimuundo zinazodhihirika katika silabi za Kiswahili Sanifu na Kiolusuba. Lugha hizi zote ni za Kibantu kwa hivyo kuna uwezekano wa kuwepo na ulinganifu katika miundo yake kwa kiasi kikubwa. Hata hivyo, kuna uwezekano kwamba baadhi ya matatizo yanayowakumba wazungumzaji wa Kiolusuba katika matumizi ya Kiswahili ni yale yanayotokana na uundaji usio sahihi wa maneno ya Kiswahili katika matumizi yake. Kwa hivyo sehemu hii itakuwa mwongozo katika sura zitakazofuata. Aidha, kama anavyoeleza Hooper (1972), silabi huchukua nafasi ya kipekee katika mabadiliko ya kifonolojia. Uchunguzi wa silabi hizo pia unawiana na msingi wa nadharia ya FZA ambao unashikilia kwamba silabi ni kiambajengo kikuu katika sheria za Mofolojia.

Kwanza kabisa ni muhimu kufafanua dhana hii ya silabi. Hyman (1975) anasema kuwa silabi ni dhana iliyo na historia ndefu sana na kwamba wanafonolojia wameihusisha na vipande sauti hasa vya kifonolojia zaidi ya vipashio vingine. Anaendelea kusema kwamba kuna uchukulizi kuwa kuna uhusiano baina ya muundo wa silabi na muundo wa neno. Hyman anaeleza ya kwamba silabi huwa na sehemu tatu yaani mwanzo, kilele na koda ambayo ndiyo mwisho wake. Kila silabi huwa na irabu kama kilele chake. Mawazo haya yameungwa mkono na Massamba na wenzake (2004). Wanaeleza kwamba silabi huwa na irabu kama kilele chake. Hata hivyo, Massamba na wenzake wanatambua kwamba kuna silabi zinazoundwa kutumia konsonanti pekee kutegemea lugha husika.

Kulingana na Crystal (1991), silabi ni kipashio cha kifonolojia kilicho kikubwa kuliko fonimu lakini kidogo kuliko neno. Kipashio hiki hueleza muundo wa kifonolojia wa neno au maneno. Silabi huweza kuwa sauti moja tu, sauti mbili au zaidi ilmuradi zitamkwe kwa mpigo mmoja.

Hooper (1972) katika Hyman (1975) anatajwa akiwa na mawazo tofauti kidogo kuhusu dhana ya silabi na neno. Kwake Hooper, silabi na muundo wa neno ni tofauti

kwa kuwa wakati mwingine sauti fulani zinapatikana katika mianzo au katikati mwa maneno lakini sio mwishoni mwa neno. Kwa mfano, lugha nyingi za Kibantu haziruhusu maneno kuishia kwa silabi funge. Maelezo haya yametumika sana katika kutambua maneno mageni hasa katika lugha ya Kiswahili Sanifu.

Kuna aina mbili za silabi; Silabi wazi na silabi funge. Silabi wazi pia huitwa silabi huru. Silabi hizi huishia kwa irabu zinapotamkwa. Kwa hivyo silabi wazi husikika zaidi kuliko silabi funge. Silabi funge huishia kwa konsonanti ambazo hukatika ghafla katika matamshi. Katika Kiswahili Sanifu, maneno yaliyo na silabi funge ni yale ya mkopo yaani yasiyo ya asili ya Kibantu.

3.1.2 Muundo wa silabi katika Kiswahili Sanifu

Kiswahili Sanifu kina miundo anuwai ya silabi ambazo huundwa kwa kuunganisha pamoja fonimu mbalimbali katika ruwaza maalum ili ziweze kutamkika. Wataalamu kama Katamba (1989), ameeleza kwamba muundo wa silabi ndio hutupa kanuni ambazo zinatawala matumizi ya lugha fulani hasa katika ile hali ya kujaribu kuleta sauti fulani pamoja ili kuunda silabi. Mgullu (2001) amejadili miundo saba ya silabi za Kiswahili Sanifu ilhali Iribemwangi (2010) ameziainisha aina tisa za miundo ya silabi za Kiswahili Sanifu. Miundo yenyewe ni kama ifuatayo.

3.1.2.1 Muundo wa silabi pendwa (KI)

Wanaisimu kama vile Crystal (1991), Hyman (1975), Mgullu (2001) wanaeleza kwamba muundo huu ndio wa msingi kabisa na wa awali kuliko miundo yote ya silabi. Aidha, muundo huu hupatikana katika takriban lugha zote ulimwenguni. Kwa hivyo katika lugha za Kibantu muundo huu huitwa muundo wa silabi pendwa. Baadhi ya maneno yenye muundo huu katika Kiswahili Sanifu ni kama:

12. /pɛ\$lɛ\$ka/

/ta\$ti\$zo/

/ru\$di\$ja/

/lɛ\$ta/

3.1.2.2 Muundo wa konsonanti konsonanti Irabu (KKI)

Muundo huu huhusisha mojawapo kati ya nazali tano katika nafasi ya kwanza, vikwamizwa au vipasuo katika nafasi ya pili na irabu yoyote katika nafasi ya mwisho. Mifano ya maneno yenye muundo huu ni kama vile:

13. /mbɔ\$ga/

/ga\$nda/

/ŋga\$no/

3.1.2.3 Muundo wa konsonanti nusu irabu Irabu (K^{1/2}II)

Katika muundo huu, konsonanti tofauti tofauti huchukua nafasi ya kwanza. Zinafuatwa na nusu irabu kisha nafasi ya mwisho huchukuliwa na irabu. Mifano ya maneno yenye muundo huu ni:

14. /mwa\$ta/

/fyε\$ka/

/kwɔ\$te/

/m\$pya/

3.1.2.4 Muundo wa konsonanti konsonanti nusu Irabu irabu (KK^{1/2}II)

Muundo huu huwa na konsonanti ya nazali katika nafasi ya kwanza. Nafasi ya pili aghalabu huchukuliwa na kipasuo kisha nusu irabu hufuata na kumaliziwa na irabu. Maneno machache tu katika Kiswahili huwa na muundo huu. kwa mfano:

15. /ŋgwε\$na/

/ja\$ngwa/

/mbwε\$ha/

/ndwε\$le/

3.1.2.5 Muundo wa Irabi pekee (I)

Katika Kiswahili kuna muundo huu ambao huwa na sauti moja tu ya irabu ikijisimamia kama silabi. Aghalabu sauti za irabu hizo hufuatana pekee bila kuungana na konsonanti katika mazingira yoyote. Zinaweza kuwa mwanzoni, katikati au mwishoni mwa neno. Mifano ya maneno yenye silabi za irabu pekee ni:

16. /ɔ\$ a/

/u \$ a/

/a \$ u/

3.1.2.6 Muundo wa konsonanti pekee (K)

Muundo huu hutokea pale ambapo konsonanti husimama pekee kama silabi bila kuungana na herufi nyingine. Hata hivyo, ni konsonanti za nazali /m/ za midomo na

/n/ za ufizi tu ndizo zimeonyesha hali hii. Sauti hizi hutokea kama silabi mwanzoni mwa neno na katikati lakini si mwishoni mwa neno. Mifano yake ni:

17. /n\$fi/

/ni\$m\$fa\$pe/

/m\$la\$ngo/

3.1.2.7 Muundo wa konsonanti irabu irabu (KII)

Huu ni muundo ambao hutokea ambapo konsonanti hufuatwa na irabu mbili. Mfuatano huu wa irabu aghalabu hudhihirika kama irabu ndefu. Katika muundo huu, nafasi ya kwanza huchukuliwa na konsonanti kisha hufuatwa na irabu ya aina moja mara mbili. Muundo huu hauna maneno mengi katika Kiswahili. Kwa mfano

18. /ma:\$fa/

/ma:\$na/

/ga:\$ga:/

/fa:/

3.1.2.8 Silabi funge

Katika muundo huu wa silabi, konsonanti huchukua nafasi ya mwisho. Muundo huu hautumiki sana katika Kiswahili na hata lugha nyingine za Kibantu. Utafiti umeonyesha ya kwamba maneno yaliyo na muundo huu wa silabi katika Kiswahili ni maneno mageni yaliyokopwa kutoka kwa lugha nyingine zisizo za Kibantu mathalani Kiingereza. Kwa mfano:

19. /dak\$ta\$ri/

/ham\$si\$ni/

Hata hivyo muundo huu unadaiwa kuwa ni ya asili ya Kiswahili na baadhi ya wanaisimu.

3.1.2.9 Muundo wa konsonanti konsonanti konsonati irabu (KKKI)

Huu ni muundo wa mfuatano wa konsonanti tatu bila kuingiliwa kati na irabu. Ni muundo ambao hudhihirika tu katika maneno ya mkopo yaliyotoholewa kutoka lugha geni. Mifano ya maneno hayo ni kama:

20. /skru\$bu/

/spri\$ngi/

3.1.3 Muundo wa silabi katika Kiolusuba

Hata ingawa Kiolusuba ni lugha ya Kibantu kama ilivyo Kiswahili, lugha hizi zina tofauti zake licha ya kuwa na sifa nyingi zinazokaribiana. Hyman (1975) anasema kuwa kila lugha ina muundo wake wa silabi. Anaendelea kueleza kwamba silabi zenyewe huundwa kwa kuleta pamoja fonimu katika mazingira fulani ili kupata ruwaza inayoweza kutamkika. Haya mawazo ni dhahiri kwamba yanasawiana na ya Crystal (1991) ambaye pia anasema kwamba kipashio hiki cha silabi hueleza muundo wa kifonolojia wa neno au maneno na huweza kuwa sauti moja mbili au zaidi ilmuradi zitamkwe kwa mpigo mmoja.

Tungependa kueleza kwamba Kiolusuba kinadhihirisha kuwa miundo ya silabi inaweza kufanana lakini mwishowe miundo ya maneno itofautiane kama anavyosema Hooper (1972) katika Hyman (1975). Hii ni kwa sababu kuna maneno mengi katika Kiolusuba yaliyo na miundo ya silabi inayofanana na miundo ya silabi katika Kiswahili Sanifu lakini maneno yenyewe yameundwa tofauti. Kwa mfano, nomino zote katika Kiolusuba huwa na kiambishi kitangulizi kabla ya kiambishi ngeli. Tuchukue kwa mfano neno [kinu] katika Kiswahili, limekaribiana sana na [Ekinu] katika Kiolusuba. Miundo ya silabi zake inasawiana lakini miundo ya maneno yenyewe ni tofauti. Miundo ya silabi katika Kiolusuba ni kama ifuatayo:

3.1.3.1 Muundo wa Konsonanti Irabu (KI)

Muundo huu ni ule wa silabi pendwa. Unadhihirika katika Kiolusuba kama ilivyo katika lugha nyingine za Kibantu na hata zisizo za Kibantu. Katika muundo huu kila konsonanti hufuatwa na irabu, Mifano ya maneno yenye muundo huu ni:

<i>Kiolusuba</i>	<i>maana</i>
21. /jɔ\$ ja/	andika
/ɛ\$ ki \$ nu/	kinu
/tɛ\$ ma/	kata
/gu \$ sa/	kunywa
/wa \$ la/	hesabu

3.1.3.2 Muundo wa Konsonanti Konsonanti Irabu (KKI)

Katika muundo huu Konsonanti za nazali huchukua nafasi ya kwanza zikifuatwa na konsonanti za vipasuo na ya mwisho huweza kuchukuliwa na mojawapo ya irabu kumi. Mifano:

<i>Kiolusuba</i>	<i>Maana</i>
22. /ε\$ n \$ si \$ <u>mb</u> ɔ/	fimbo
/ ε\$ <u>ngi</u> \$ ra/	ingia
/ε\$ m \$ pa \$ <u>nga</u> /	jogoo
/ɲi \$ <u>ngε</u> : \$ nɔ/	saa hii

3.1.3.3 Muundo wa konsonanti irabu irabu (*KK^{1/2}I I*)

Katika muundo huu, konsonanti huafuatwa na nusu irabu na kisha hufuatwa na irabu.

Muundo huu hudhihirika sana katika Kiolusuba. Mifano ya maneno yaliyo na muundo huu ni kama:

<i>Kiolusuba</i>	<i>Maana</i>
23. /fwa\$na\$na/	fanana
/ε\$ m \$ pa \$ <u>nwa</u> /	zawadi
/ɔ\$ lu \$ <u>ywi</u> \$ ri/	unywele
/a \$ ma\$ <u>twi</u>	vichwa
/a \$ wa \$ mb /\$ <u>rwe</u>	asulubishwa
/ɔ\$ wu \$ <u>lwi</u> \$ rε/	ugonjwa

3.1.3.4 Muundo wa konsonanti konsonanti nusu irabu irabu (*KK^{1/2}II*)

Huu ni muundo ambao hutokea kwa kutangulizwa kwa konsonanti ya nazali ikifuatwa na konsonanti ya mtuo kisha nusu irabu na mwishowe irabu. Muundo huu una maneno machache sana katika Kiolusuba.

<i>Kiolusuba</i>	<i>Kiswahili</i>
24. /mbwε/	eti
/ε\$ nswa/	nyungu
/ε\$ mbwa/	mbwa

3.1.3.5 Muundo wa irabu pekee (*I*)

Muundo huu upo katika Kiolusuba na hujitokeza kwa maneno mengi mbali na ilivyo katika Kiswahili. Nomino zote hutangulizwa kwa irabu inayojisimamia kama silabi.

Pia kuna maneno ambayo yana silabi za irabu. Kwa mfano:

<i>Kiolusuba</i>	<i>maana</i>
25. /a\$ ri \$ <u>ɔ</u> \$ ga /	ataoga
/ɔ\$ nɔ/	huyo

/ri \$a\$ ɔ/

lao

3.1.3.6 Muundo wa konsonanti pekee (K)

Muundo huu wa silabi huweza kumithilishwa na ule muundo wa silabi funge katika Kiswahili ulio wa maneno mageni. Katika Kiolusuba, muundo huu hujitokeza katika maneno asilia.

Kiolusuba

26. /ɛ\$ n\$ zɔ\$vu/

/r\$ ra/

/ɔ\$ mu \$ r\$ rɔ/

Kiswahili

ndovu

lia

moto

3.1.3.7 Muundo wa Konsonanti Irabu Irabu (KII)

Muundo huu tofauti na ulivyo katika Kiswahili hutokea katika maneno mengi mno. Sababu ni kwamba unadhihirika hasa katika irabu ndefu. Kama tulivyoona awali ni kwamba irabu zote za Kiolusuba hutokea kama irabu ndefu na za kwaida. Zaidi ya hayo, tuliona kwamba kuna maneno ya asili ya Kiolusuba chungu nzima yaliyo na irabu ndefu pamoja na maneno yote mageni yanayoingizwa katika Kiolusuba. Mifano yake ni:

Kiolusuba

27. /a\$ ma: \$ ni /

/re: \$ rɔ/

/ge: \$ za/

/a\$ mi: \$ sɔ/

/a\$ ma: \$ tɔ/

Kiswahili

nguvu

leo

nzuri

macho

mitumbi

3.1.3.8 Muundo wa Konsonanti Konsonanti Konsonanti Irabu (KKKI)

Katika muundo huu silabi huundwa na sauti tatu za konsonanti mfululizo kisha hufuatishwa na irabu. Muundo huu wa KKKI unadhihirika katika maneno ya kiasili ya Kiolusuba ijapokuwa kwa maneno machache.

Kiolusuba

28. /gi \$ ngre/

/fu\$ mbra/

Kiswahili

bebea

pikia

3.1.3.9 Muundo wa nusu Irabu Irabu (½II)

Muundo huu ni ule unaohusisha nusu Irabu /w/ na /j/ zikifuatwa na irabu zozote. Muundo huu hata ingawa haujaratibishwa katika miundo ya Kiswahili, unastahili kuchunguzwa na kuongezewa humo. Mifano ya maneno yaliyo na muundo huu ni:

<i>Kiolusuba</i>	<i>Kiswahili</i>
29. /ɔ\$wɔ\$ i\$ ta /	ugali
/ɔ\$wɔ\$ se\$ ra/	uji

Pia, kuna muundo wa nusu irabu irabu irabu (½ I I I) katika Kiolusuba. Kwa mfano:

30. /wɔ:na/	wote
/ya:\$ ε/	yake
/wa:\$ ε/	wake

Hata ingawa maneno ambayo yana muundo huu katika Kiswahili yanaratibiwa pamoja na KI, ni makosa kwani lau tunatambua K½II, tunastahili kutambua ½ I I pia. Kwa mfano maneno kama:

31. /yu\$a\$ja /
/wɔ\$te/
/wa:\$ma/

3.1.4 Ulinganishi na ulinganuzi wa miundo ya silabi za Kiswahili Sanifu na Kiolusuba

Lugha hizi mbili zina asili moja kwani zote zilitokana na Mame Bantu. Kwa hivyo kwa kiwango kikubwa zinawiana katika mifumo yake ya silabi. Hata hivyo hakuna lugha mbili zinazofanana katika kila hali. Hivyo kuna tofauti chache hapa na pale.

Kama anavyotaja Hyman (1975) kwamba lugha zote zina muundo wa silabi pendwa KI. Muundo huu upo katika lugha zote mbili kama inavyodhihirika katika maneno yafuatayo.

<i>Kiolusuba</i>	<i>maana</i>	<i>Kiswahili</i>
32. /ku\$ba/	piga	/tɔ\$ka/
/jɔja /	andika	/ru\$di/

Lugha hizi zote zina muundo wa KKI ambapo pana mfuatano wa konsonanti mbili zikifuatwa na irabu. Muundo huu unajitokeza katika maneno kama haya:

<i>Kiolusuba</i>	<i>maana</i>	<i>Kiswahili</i>
33. /ε\$mbu\$ zi/ /ɔ\$wa\$wa:\$nga/	mbuzi alikuwepo	/ngu\$zɔ/ /tε\$ mbε\$ a/

Tukiangalia muundo wa K ½ I I, tunaona kwamba unapatikana katika lugha zote mbili kama inavyodhihirika katika maneno yafuatayo.

<i>Kilolusuba</i>	<i>maana</i>	<i>Kiswahili</i>
34. /ɔ\$lu\$ywi\$ri/ /fwa\$ na \$ na/	unywele fanana	/m\$pya/ /fyε\$ ka/

Vilevile, ule muundo wa **KK1½II** pia unajitokeza katika lugha hizi japo katika maneno machache mno. Mifano:

<i>Kiolusuba</i>	<i>maana</i>	<i>Kiswahili</i>
35. /mbwε/ /ε\$ nswa/	eti nyungu	/mbwε\$ha/ /ndwε\$le/

Kuna muundo wa irabu pekee katika lugha hizi mbili ambao umedhihirika katika maneno kama yafuatayo.

<i>Kiolusuba</i>	<i>maana</i>	<i>Kiswahili</i>
36. /ya:\$ ε/ /ɔ\$ nɔ/	yake huyu	/ɔ\$ a/ /u\$ a/

Pia, kuna muundo wa konsonanti pekee umeonekana kwenye baadhi ya maneno katika kila upande. Mifano ya maneno hayo ni kama ifuatayo

<i>Kiolusuba</i>	<i>maana</i>	<i>Kiswahili</i>
37. /ɔ\$ mu \$ r\$ rɔ/ /ε\$ n\$ zɔ\$ vu/	moto ndovu	/ni \$m\$ ffa\$pe/ /n\$ fi/

Muundo wa KII pia umejitokeza katika lugha hizi mbili. Mifano ya maneno katika kila lugha ni kama:

<i>Kiolusuba</i>	<i>maana</i>	<i>Kiswahili</i>
38. /a\$ ma:\$ ni/ /rε:\$ rɔ/	nguvu leo	/ma:\$fa/ /ga:\$ ga:/

Muundo wa KKKI unafahamika kwamba si wa kawaida katika baadhi ya lugha za Kibantu mathalani Kiswahili, unadhihirika kwa maneno kopwa tu kama vile ya Kiingereza. Katika Kiolusuba, silabi hii ipo hasa katika uambishaji wa vitenzi katika kauli mbalimbali ila kwa maneno machache mno.

<i>Kiolusuba</i>	<i>maana</i>	<i>Kiswahili</i>
39. /a\$gi\$ngre/	ambebee	/skru\$bu/
/a\$wu\$a\$mbre/	asulubishe	/spri\$ngi/

3.1.5 Ulinganuzi wa miundo ya silabi katika Kiolusuba na Kiswahili Sanifu
Ulinganifu umeonekana ni mwingi kwa kuzingatia mifumo ya silabi ya lugha hizi mbili. Hata hivyo kuna baadhi ya sehemu zinazotofautiana. Katika Kiswahili, silabi za konsonanti pekee huwa ni nazali za mdomo /m/ na sauti za ufizi /n/ pekee ndizo zinaweza kujisimamia kama silabi ilhali katika Kiolusuba hata sauti ya ufizi /r/ isiyo ya nazali huweza kujisimamia kama silabi. Kwa mfano:

<i>Kiolusuba</i>	<i>maana</i>
40. /r\$ ra /	lia
/o\$ mu \$r\$ rɔ/	moto

Upeo wa kudhihirika kwa muundo wa KKK katika Kiswahili ni mfinyu ukilinganishwa na Kiolusuba kwa kuwa unadhihirika katika maneno kopwa ilhali Kiolusuba kina muundo huo katika maneno yake asilia. Kwa mfano:

<i>Kiolusuba</i>	<i>maana</i>
41. /gi\$ngre/	bebea
/fu\$mbra/	pikia

Aidha, hata ingawa inaelekea kwamba muundo wa ½ I I haitambuliki katika Kiswahili labda kwa kuzingatia mifanyiko ya kifonolojia kwamba /u/ huyeyushwa na kuwa /w/ na /i/ kuwa /y/. Katika Kiolusuba sauti hizi zinajitokeza katika maneno mengi na hivyo kuunda silabi ambazo hazipo katika Kiswahili Sanifu. Hata ingawa fonimu /j/ pamoja na /u/ zinaunda silabi katika Kiswahili /w/ na /u/ hazitumiki kwa pamoja kuundia silabi kama inavyodhihirika aghalabu zikifuatana katika Kiolusuba. Mifano katika Kiolusuba ni:

<i>Kiolusuba</i>	<i>maana</i>
42. /o\$wu\$ se\$ra/	uji
/o\$wu\$si \$ ta/	ugali
/wu\$a\$ ε/	wake

Hata hivyo muundo wa /j/ ikifuatwa na /u/ hutumika sana katika Kiswahili. Kwa mfano:

43. /yu\$m\$ki\$ni/

/yu\$le/

3.2 Hitimisho

Ulinganifu upo kwa kiwango kikubwa baina ya lugha hizi mbili kwa kuzingatia miundo ya silabi. Tofauti pia ipo bali ni kwa kiwango kidogo tu. Ikumbukwe kwamba lugha hizi mbili zinaweza kukaribiana kutokana na ukweli kwamba zote ni lugha za Kibantu ambazo zina mifumo ya sauti inayokaribiana kutokana na hali kwamba zote zilitokana na Mame Bantu.

4. SURA YA NNE

4.1 NOMINO NGELI ZA KISWAHILI SANIFU NA KIOLUSUBA

4.1.1 Utangulizi

Katika sura hii, tutazibainisha ngeli nomino za Kiswahili Sanifu na Kiolusuba huku tukionyesha viambishi vinavyotumika katika uainishaji wa ngeli pamoja na mifano ya nomino zinazopatikana katika kila ngeli. Aidha, tutaonyesha jinsi nomino hizo zinavyoathirika na baadhi ya mifanyiko ya kifonolojia. Kama tulivyosema awali, uainishaji wa majina katika ngeli ndiyo sifa kuu inayozitambulisha lugha za Kibantu. Kuna namna tatu kuu za kuainisha ngeli nomino katika Kiswahili. Njia hizo ni za kimofolojia, kisintaksia na kisemantiki. Hata hivyo, Iribemwangi (2010) amependekeza njia ya nne ambayo inajumuisha njia hizo tatu.

Katika Kiolusuba, ngeli zimeshughulikiwa kimofolojia. Hii ndiyo njia iliyotumika katika uchunguzi wa lugha za Kibantu tangu jadi kama anavyoeleza Iribemwangi akiwataja wanaisimu kama vile Bleek (1869). Mwelekeo huu wa kimofolojia ndio uliochukuliwa na wanaisimu kama Polome (1967) kama wanavyoeleza Kihore na wenzake (2001). Utafiti huu umetumia uainishaji wa kimofolojia kushughulikia uainishaji wa nomino ngeli za lugha hizi mbili. Uchunguzi tulioufanya uligundua kwamba Kiolusuba kina ngeli kumi na saba. Nomino za Kiolusuba zina viambishi vitangulizi ambavyo hufuatwa na viambishi vibainishi vya ngeli. Jedwali katika ukurasa unaofuata linaonyesha ngeli za Kiolusuba.

Nomino ngeli za Kiswahili Sanifu

Uainishaji wa ngeli za Kiswahili Sanifu kimofolojia unatambua ngeli kumi nane.

Ngeli hizo ni pamoja na:

Ngeli 1{mu-}

Majina katika ngeli hii huchukua nomino zenye kiambishi {mu-}. Mifano ya nomino katika ngeli hii ni:

44. /mu+tu/ [mtu]

/mu+tɔtɔ/ [mtɔtɔ]
/mu+ana/ [mwana]

Ngeli 2 {wa-}

Ngeli hii huwakilisha wingi wa ngeli ya kwanza. Kiambishi ngeli cha ngeli hii ni {wa-}. Mifano ya nomino katika ngeli hii ni:

45. /wa+tɔtɔ/ [watɔtɔ]
/wa+alimu/ [walimu]
/wa+ana/ [wana]

Ngeli 3 {mu-}

Nomino katika ngeli hii huchukua kiambishi {mu-}. Kiambishi hiki kina alomofu {mu-} na {mw-}. Mifano ya nomino zake ni:

46. /mu+undɔ/ [muundɔ]
/mu+ti/ [mti]
/mu+langɔ/ [mlangɔ]
/mu+iba/ [mwiba]

Ngeli 4 {mi-}

Ngeli hii ni ya wingi wa nomino zinazopatikana katika ngeli ya 3. Mofu ya kiambishi ngeli hii ni {mu-} na haina alomofu. Baadhi ya nomino katika ngeli hii ni:

47. /mi+undɔ/ [miundɔ]
/mi+ti/ [miti]
/mi+langɔ/ [milangɔ]
/mi+ba/ [miba]

Ngeli 5 {ji- /ϕ-}

Nomino nyingine katika ngeli hii huwa na kiambishi {ji-} na nyingine mofu {ϕ-}. Mifano ya nomino hizi ni pamoja na:

48. /ϕ+tawi/ [tawi]
/ji+ʃɔ/ [matʃɔ]
/ϕ+gɔti/ [magoti]

Ngeli 6 {ma-}

Ngeli hii huwakilisha wingi wa ngeli ya tano. Kiambishi cha ngeli hii hudhihirika hata katika nomino ambazo huwa na mofu kapa katika ngeli ya tano. Kwa mfano:

49. /ma+ʃɔ/	[maʃɔ]
/ma+gɔti/	[magɔti]
/ma+tawi/	[matawi]

Ngeli 7{ki-}

Ngeli hii ina mofimu {ki-} kama kiambishi chake. Mofimu ya ngeli {ki-} huwa na alomofu {ʃ-}. Baadhi ya nomino katika ngeli hii ni:

50. /ki+ti/	[kiti]
/ki+atu/	[kiatu]
/ʃakula/	[ʃakula]

Ngeli 8 {vi-}

Hii huwakilisha wingi wa ngeli ya saba na mofu ngeli yake ni {vi-}. Alomofu ya ngeli hii ni {vj-}. Mifano ya nomino za ngeli hii ni:

51. /vi+atu/	[viatu]
/vi+akula/	[vjakula]
/vi+ti/	[viti]

Ngeli 9{n/ ɸ}

Hakuna kiambishi ngeli maalumu kinachowakilisha ngeli hii. Nomino za ngeli hii huendelezwa sawa katika umoja na wingi wake. Wataalamu kama vile Carl Meinhof wanatudokezea kwamba ngeli hii ilikuwa na kiambishi {n-} ambayo ilidondoshwa kimapisi na kuacha shina la neno tu. Kwa mfano:

52. /n+kalamu/	[kalamu]
/n+meza/	[meza]
/n+pete/	[pete]

Ngeli 10{n/φ-}

Ngeli ya 9 na 10 zinadhihirika kwa njia sawa kimofolojia. Tofauti baina yake huonekana katika upatanisho wa kisarufi kama wanavyosema Habwe na Karanja (2004). Kwa mfano: *Nywele ndefu zimenyolewa.*

Ngeli 11{u-}

Nomino zinazopatikana katika ngeli hii huwa na kiambishi ngeli {u-}. Kiambishi {u-} kina alomofu {w-}. Mifano ya nomino katika ngeli hii ni:

53. /u+dɛvu/	[udɛvu]
/u+jia/	[ujia]
/u+ɛmbɛ/	[wɛmbɛ]
/u+araka/	[waraka]

Ngeli hii hupata wingi wake katika ngeli ya 10.

Ngeli ya 12 na 13 ambazo zina viambishi {ka-} na {tu-} mtawalia hazitambuliwi katika Kiswahili Sanifu.

Ngeli 14 {u-}

Kiambishi cha ngeli hii ni {u-}. Nomino katika ngeli hii aghalabu ni zile zilizo dhahania. Kwa mfano:

54. /u+gɔnjwa/	[ugonjwa]
/u+tukufu/	[utukufu]
/u+zuri/	[uzuri]

Ngeli 15 {ku-}

Ngeli hii ni ya vitenzi vinavyofanya kazi kama nomino. Nomino hizo hudhihirika kimatumizi. Kwa mfano : *Kuimba kwake kunapendeza.* Mifano ya nomino vitenzi vingine ni kama vile:

55. /ku+ʃɛza/	[kuʃɛza]
/ku+iga/	[kuiga]
/ku+soma/	[kusoma]

Ngeli ya 16, 17 na 18 {pa, ku, mu}

Ngeli hizi hurejelea mahali mbali mbali za mahali. Ngeli ya 16 huwa na kiambishi ngeli {pa-}. Hii ni ngeli inayoonyesha mahali kamili au mahususi kwa mfano *hapa.*

Mofimu ya ngeli ya 17 ni {ku-}. Ngeli hii huonyesha ujumla wa mahali kama vile *huku*.

Mofimu ya ngeli ya 18 ni {mu-}. Ngeli hii huonyesha undani wa mahali. Kwa mfano *humu ndimo tunamoishi*.

Kielelezo 4.1 Jedwali la ngeli za Kiolusuba

Nambari	Ngeli	Mifano ya nomino	maana
1	{ɔmu-} {ɔmw-}	omuntu, omugerezi, omurimi omwiko, omwami, omwana	mtu, mwalimu, mkulima fafiki, mfalme, mtoto
2	{awa-}	awantu, awagerezi, awarimi awiiko, awaami, awaana	Watu, walimu, wakulima rafiki, wafalme, watoto
3	{ɔmu-} {ɔmw-}	omuti, omutwe, omusiri omwoyo	ti, kichwa, shamba moyo
	{ɔgu-}	ogugombe, oguuzi, ogubwa	gombe, buzi, jibwa
	{ugu-}	uguntu, uguti,	jitu, jiti
4	{ɛmi-}	emiti, emitwe, emisiri, emioyo	miti, vichwa, mashamba, mioyo
5	{ɛri-} ϕ	eriiso, eriino, eriina igosi, ing'ana, igi	jicho, jino, jina shingo, neno, yai
6	{ama-}	amiiso, amiino, amiina amagi, amangana, amagi	macho, meno, majina shingo, neno, yai
7	{ɛki-}	ekiratu, ekituutu, ekinu	kiatu, ushanga, kinu
8	{ɛwi-}	ewiratu, ewituutu, ewinu	viatu, tarumbeta, vinu
9	{ɛN-}	entewe, entikiri, embuzi	kiti, punda, mbuzi
10	{ɛN-}	entewe, entikiri, emuzi	viti, punda, mbuzi
11	{ɔlu-}	oluvwiri, oluwago, olutare	unywele, ua, mwamba
12	{aka-}	akantu, akati, akabwa	kijitu, kijijiti, kijibwa
13			
14	{ɔwu-}	owuato, owusera, owuswi	mtumbi, uji, nyasi
15	{ɔku-}	okusesa, okumenya, okusemera	Kupepeta, kuishi, kudanganya
16			
17	{ku-}	Kunyumba,	nyumbani
18	{mu-}	Munyumba, musukuuli	Ndani ya nyumba, ndani ya shule

4.1.1.1 Ngeli ya 1 {ɔmu-}

Ngeli ya kwanza katika Kiolusuba huchukua mofu {ɔmu-} ambayo huwakilisha hali ya umoja. Majina katika ngeli hii ni ya binadamu tu katika hali ya wastani au kawaida. Kiambishi cha ngeli hii kina alomofu mbili yaani {ɔmu-} na {ɔmw-}. Mifano ya majina katika ngeli hii ni:

Nomino	Mnukuu	maana
56. /ɔmu+ntu/	[ɔmuntu]	mtu
/ɔmu+lɔzi/	[ɔmulɔzi]	mlozi
/ɔmu+sa:za/	[ɔmusa:za]	mume
/ɔmu+kazi/	[ɔmuka:zi]	mke
/ɔmu+gɛɾɛzi/	[ɔmugɛɾɛzi]	mwalimu
/ɔmu+ikɔ/	[ɔmwikɔ]	rafiki
/ɔmu+ana/	[ɔmwana]	mtoto
Alomofu za {ɔmu-} $\left\{ \begin{array}{l} \{ɔmu-\} \\ \{ɔmw-\} \end{array} \right.$		

4.1.1.2 Ngeli ya 2 {awa-}

Ngeli hii ni ya wingi wa maneno katika ngeli ya kwanza. Kiambishi cha ngeli hii ni {awa}. Kulingana na Guthrie (1947), lugha za Kibantu huchukuwa {ba-} ya kihistoria kama kiambishi cha ngeli ya pili. Mawazo hayo yanaungwa mkono na Polome (1967). Kwa hivyo, katika Kiolusuba, kiambishi [awa-] ni udhoofishaji wa kiambishi {aβa-} kutokana na kile kiambishi {ba-} cha kihistoria. Swaleh (2005) anapendekeza kwamba udhoofishaji ule ungechukua mwelekeo huu katika lugha zinazotumia {wa-} kama kiambishi cha ngeli hii.

[b] → [β] → [w] au

[b] → [v] → [β] → [w]

Kwa kuwa /b/ ni kipasuo kinachohitaji nguvu nyingi katika kutamka kuliko kikwamizwa /β/, ni dhahiri kwamba kiambishi {awa-} kinatokana na udhoofishaji wa /aβa/. Mifano ya nomino za ngeli ya pili ni:

Nomino	Mnukuu	maana
57. /awa+ntu/	[awantu]	watu
/awa+lɔzi/	[awalɔzi]	walogi
/awa+sa:za/	[awasa:z]	wanaume

/awa+kazi/	[awakazi]	wanawake
/awa+gɛɛɛzi/	[awagɛɛɛzi]	walimu
/awa+sakuzi/	[awasakuzi]	wezi
/awa+ana/	[awa:na]	watoto
/awa+ala/	[awa:la]	wasichana
/awa+ikɔ/	[awi:kɔ]	marafiki

4.1.1.3 Ngeli ya 3 {ɔmu-}

Nomino mbalimbali zinapatikana katika ngeli hii katika hali ya umoja. Baadhi ya majina yanayopatikana hapa ni pamoja na majina ya mimea, sehemu za mwili na majina ya vitu asili kama anavyoeleza Polome (1967:97). Kiambishi cha Ngeli hii ni {ɔmu-}. {ɔmu-} na {ɔmw-} ni alomofu. Mifano ya nomino zinazopatikana katika ngeli hii ni:

Nomino	Mnukuu	maana
58. /ɔmu+ti/	[ɔmuti]	mti
/ɔmu+twɛ/	[ɔmutwɛ]	kichwa
/ɔmu+kɔɔɔ/	[ɔmukɔɔɔ]	mkono
/ɔmu+siri/	[ɔmusiri]	shamba
/ɔmu+ɔjɔ/	[ɔmwojɔ]	moyo

Pia, ngeli hii hujumuisha nomino katika hali ya ukubwa. Kiambishi cha nomino katika hali ya ukubwa ni:

{ugu-}. Ngeli hii kwa hivyo ni **ngeli ya 3a** Mifano ya nomino katika ngeli hii ni:

Nomino	Mnukuu	maana
59. /ugu+ntu/	[uguntu]	jitu
/ugu+ti:/	[uguti:]	jiti
/ɔgu+gɔmbɛ/	[ɔgugɔmbɛ]	gombe
/ɔgu+uzi/	[ɔgu:zi]	buzi
/ɔgu+bwa/	[ɔgubwa]	jibwa

Alomofu za kiambishi ngeli hii ni {ɔgu-} na {ugu-}

4.1.1.4 Ngeli ya 4 {emi-}

Majina katika ngeli ya nne aghalabu huwa majina ya wingi wa ngeli ya tatu. Kiambishi cha ngeli hii ni {emi-}. Baadhi ya majina yanayopatikana katika ngeli hii ni kama yafuatayo:

Nomino	Mnukuu	maana
60. /emi+ti/	[ɛmiti]	miti
/emi+twɛ/	[ɛmitwɛ]	vichwa
/emi+siri/	[ɛmisiri]	mashamba
/emi+ɔjɔ/	[ɛmiɔjɔ]	mioyo
/emi+ntu/	[ɛmintu]	majitu
/emi+bwa/	[ɛmibwa]	majibwa

4.1.1.5 Ngeli ya 5 {eri- /ϕ}

Ngeli hii ina majina ya aina mbalimbali yakiwemo majina ya viungo vya mwili, viumbe vya asili pamoja na majina ya baadhi ya wanyama. Kiambishi cha ngeli hii ni {eri-}. Kiambishi hiki kina alomofu kapa {ϕ} kama inavyojitokeza katika mifano hii:

Nomino	Mnukuu	maana
61. /eri+i+sɔ/	[ɛri:sɔ]	jicho
/eri+i+nɔ/	[ɛri:nɔ]	jino
/eri+i+na/	[ɛri:na]	jina
/ϕ+i+gɔsi/	[igɔsi]	shingo
/ϕ+i+gɛsa/	[igɛsa]	mavuno
/ϕ+i+gi/	[igi]	yai
/ϕ+i+gugɛ/	[igugɛ]	tumbiri
/ϕ+i+saka/	[isaka]	kichaka
/ϕ+i+gɔndi/	[igondi]	kondoo

4.1.1.6 Ngeli ya 6 {ama-}

Hii ni ngeli ya wingi wa nonino za ngeli ya tano. Polome (1967) anasema kuwa ngeli hii inajumuisha hata majina ya vitu viowevu kama vile maji, mafuta na mengineyo. Kiambishi cha ngeli hii ni {ama-}. Majina yanayopatikana katika ngeli hii ni pamoja na:

Nomino	Mnukuu	maana
62. /ama+isɔ/	[ami:sɔ]	macho
/ama+inɔ/	[ami:nɔ]	meno

/ama+ina/	[ami:na]	majina
/ama+tɔkε/	[amatɔke]	ndizi
/ama+i+saka/	[amasaka]	vichaka
/ama+i+na/	[ami:na]	majina
/ama+i+gi/	[amagi]	mayai
/amanzi/	[amanzi]	maji
/amavuta/	[amavuta]	mafuta

4.1.1.7 Ngeli ya 7 {εki-}

Nomino katika ngeli hii huchukua kiambishi ngeli cha {εki-} katika hali ya umoja. Baadhi ya majina yanayopatikana katika ngeli hii ni ya vitu visivyo na uhai, wanyama na hata majina ya lugha na vyombo mbalimbali. Mifano ya nomino katika ngeli hii ni:

Nomino	Mnukuu	maana
63. /εki+ratu/	[εkiratu]	kiatu
εki+ti:ti/	[εkiti:ti]	ushanga
/εki+tu:tu/	[εkitu:tu]	tarumbeta
/εki+nu/	[εkinu]	kinu
/εki+iti/	[εkiti]	kijitu
/εki+kapu/	[εkikapu]	kikapu
/εkisuusu/	[εkisuusu]	sungura

4.1.1.8 Ngeli ya 8 {εwi-}

Majina yanayopatikana katika ngeli hii ni ya wingi wa majina ya ngeli ya saba. Kiambishi cha ngeli hii ni {εwi-}. Kwa mfano:

Nomino	Mnukuu	maana
64. /εwi+ratɔ/	[εwiratɔ]	viatu
/εwi+ti:ti/	[εwiti:ti]	shanga
/εwi+tu:tu/	[εwitu:tu]	tarumbeta
/εwi+ntu/	[εwintu]	vijitu
/εwi+ti /	[εwiti]	vijiti
/εwi+kapu/	[εwikapu]	vikapu
/εwi+susu/	[εwisusu]	sungura

4.1.1.9 Ngeli ya 9 {εN-}

Kiambishi cha ngeli nomino hii ni {εN-}. Majina katika ngeli hii inajumuisha nomino nyingi za kawaida pamoja na majina ya wanyama mbalimbali. Mifano ya nomino za ngeli hii ni:

Nomino	Mnukuu	maana
65. /εN+gɔmbɛ/	[εŋɔmbɛ]	ng'ombe
/εN+gɔlbɔŋgɔlbɔ/	[εŋgɔlbɔŋgɔlbɔ]	baiskeli
/εN+buzi/	[ɛmbuzi]	mbuzi
/εN+sɛkɛ/	[ɛnsɛkɛ]	chawa
/εN+tewe/	[ɛntɛwɛ]	kiti
/εN+tikiri/	[ɛntikiri]	punda
/εN+bwa/	[ɛmbwa]	mbwa
/εN+ŋgɔkɔ/	[εŋgɔkɔ]	kuku
/εN+iɔno/	[εɾɔni]	ndege

Alomofu za { εN-} ni {εm-} , {εn-}, {εŋ-} na {εɾ}.

4.1.1.10 Ngeli ya 10

Ngeli hii inawakilisha wingi wa nomino za ngeli ya tisa. Hata hivyo, kwa kuwa nomino za ngeli ya tisa hazibadiliki katika hali ya wingi, nomino katika ngeli ya tisa ndizo zile zile za ngeli ya kumi.

4.1.1.11 Ngeli ya 11 {ɔlu-}

Nomino katika ngeli hii ni zile zinazotangulizwa kwa kiambishi {ɔlu-}. Majina mengi katika ngeli hii huwa na sifa ya wembamba au urefu lakinilsi yote. Mifano ya majina katika ngeli hii ni kama vile:

Nomino	Mnukuu	maana
66. /ɔlu+kɔ/	[ɔlukɔ]	aina ya mchezo
/ɔlu+tare/	[ɔlutare]	mwamba
/ɔlu+wagɔ/	[ɔluwagɔ]	ua
/ɔlu+vwiri/	[ɔluvwiri]	unywele

Ngeli hii hupata wingi wake katika **ngeli ya 10**. Mifano ya nomino zake ni:

Nomino	Mnukuu	maana
67. /ɛnt +ukɔ/	[ɛntukɔ]	wingi wa oluko

/ent+arɛ/	[ɛntarɛ]	miamba
/ɛm+bagɔ/	[ɛmbagɔ]	nyua
/ɛm+vwiri/	[ɛmɔvwiri]	nywele

4.1.1.12 Ngeli ya 12 {aka-}

Katika Kiolusuba, majina yanaweza kuwekwa katika hali ya udogo au hali ya kudunishwa. Majina haya yanapatikana katika ngeli ya kumi na mbili. Kiambishi cha ngeli hii ni {aka-}. Mifano ya maneno katika ngeli hii ni:

Nomino	Mnukuu	maana
68. /aka+ntu/	[akantu]	kijitu
/aka+ti/	[akati]	kijiti
/aka+bwa/	[akabwa]	kijibwa
/aka+uzi/	[akauzi]	kibuzi
/aka+gɔmbɛ/	[akagɔmbɛ]	kigombe

Nomino za ngeli hii hupata wingi wake katika **ngeli ya 7** kama tunavyoonyesha hapa chini

Nomino	Mnukuu	maana
69. /ɛwi+ntu	[ɛwintu]	vijitu
/ɛwi+ti/	[ɛwiti]	vijiti
/ɛwi+bwa/	[ɛwibwa]	vijibwa
/ɛwi+uzi	[ɛwiuzi]	vibuzi
/ɛwi+gɔmbɛ/	[ɛwigɔmbɛ]	vigombe

4.1.1.13 Ngeli ya 14 {ɔwu-}

Kiambishi cha ngeli hii ni {ɔwu-}. Ni ngeli ya majina mbalimbali pamoja na majina dhahania. Mifano ya majina katika ngeli hii ni:

Nomino	Mnukuu	maana
70. /ɔwu+atɔ/	[ɔwuatɔ]	mtumbi
/ɔwu+ita/	[ɔwuita]	ugali
/ɔwu+lɔ:tu/	[ɔwulɔ:tu]	uzuri
/ɔwu+wiji/	[ɔwuwiji]	ubaya

Baadhi ya majina katika ngeli hii hayana hali ya wingi. Kwa mfano:

Nomino	Mnukuu	maana
71. /ɔwu+sɛra/	[ɔwusera]	uji
/ɔwu+swi/	[ɔwuswi]	nyasi
/ɔwu+ti/	[ɔwuti]	woga

Hata hivyo nomino nyingine katika ngeli hii hupata hali ya wingi katika **ngeli ya 6** sita. Kwa mfano:

Nomino	Mnukuu	maana
72. /ama +atɔ/	[amatɔ]	mitumbi
/ama+ita/	[amita]	ugali

4.1.1.14 Ngeli ya 15 {ɔku-}

Ngeli hii ni ya vitenzi vinavyofanya kazi kama nomino. Kwa hivyo nomino hizi hudhihirika kimatumizi. Kiambishi cha ngeli hii ni {ɔku-}. Mifano ya nomino zinazopatikana katika ngeli hii ni:

Nomino	Mnukuu	maana
73. /ɔku+sɛsa/	[ɔkusesa]	kupepeta
/ɔku+mɛpa/	[ɔkumɛpa]	kuishi
/ɔku+sɛmɛra/	[ɔkusemɛra]	kudanganya

Mfano katika sentensi ni: “*Okumenya okulootu ne okugonzia.*” Maana yake ni: “*Kuishi kuzuri ni kupendana.*”

4.1.1.15 Ngeli ya mahali

Kiolusuba kina ngeli mbili za mahali. Ngeli inayoonyesha mahali kwa ujumla na inayoonyesha undani wa kitu. Ngeli za Kiolusuba za mahali ni ngeli ya 17 na ya kumi na nane.

a. Ngeli ya 17

Kiambishi cha ngeli hii ni {ku-} Ngeli hii huonyesha mahali kwa jumla. Kwa mfano:

Nomino	Mnukuu	maana
74. /ku+ɛ+ɲumba/	[kupumba]	nyumbani
/ku+ɛ+mɛ:sa/	[kumɛ:sa]	mezani

Tunaweza kusema “*Omuntu ari kunyumba*” kumaanisha kwamba mtu yuko kule nyumbani.

b. Ngeli ya 18

Mofu ya ngeli hii ni {**mu-**}. Hii huonyesha undani wa mahali. Kwa mfano:

75. /mu+ε+suku:li/ [musuku:li] ndani ya shule

/mu+ε+ɲumba/ [muɲumba] ndani ya nyumba

“*Omuntu ari munyumba*” Hii ina maana kwamba mtu yuko mle nyumbani. Kwa mfano:

4.1.2 Ulinganishi wa mifanyiko ya kimofonolojia katika Kiswahili na Kiolusuba

Mifanyiko ya kifonolojia ni mabadiliko mbalimbali yanayotokea wakati ambapo fonimu mbalimbali huwekwa pamoja ili kuunda vipashio vikubwa zaidi kuliko fonimu zenyewe. Vipashio hivyo vinavyoundwa ni silabi, mofu na maneno. Mabadiliko aghalabu hutokana na kuathiriana kwa fonimu mbalimbali katika mazingira ya ujirani hasa wakati zinapotakwa kwa mfululizo. Hyman (1975) anasema kuwa mabadiiko ya kifonolojia huhusu kipande sauti ambacho hupata sifa mpya au mabadiliko katika mazingira fulani. Kwa hivyo, tunapochunguza mabadiliko katika Kiswahili na Kiolusuba tunarejelea vipengele vinne vikuu.

- a. Kile kinachobadilika
- b. Kinabadilika na kuwa nini au matokeo ya mabadiliko hayo
- c. Kinachosababisha mabadiliko au mazingira
- d. Upeo wa mabadiliko hayo katika Kiolusuba

Tutaongozwa na nadharia ya FZA ambayo mihimili yake ni kanuni ya uasilia kamili na kanuni ya ujumlishaji sahihi ambazo zinajitokeza katika aina nne za sheria ambazo ni sheria za ‘P’, Mp, ‘Via’ na ‘Sandhi’. Sheria hizi ndizo zitaonyesha motisha za mifanyiko tutakayoishughulikia. Aidha, kazi hii itaonyesha miundo ndani na miundo nje ya maneno kama anavyoeleza Hooper (1976) kwamba miundo ndani hudhihirika katika miundo nje ya maneno. Hyman (1975) anaeleza kwamba katika mabadiliko ya kifonolojia, lazima mambo yafuatayo yazingatiwe ili kupambanua miundo ndani ya maneno.

1. Uwezekano wa kubashirika
2. Iktisadi ya vipashio
3. Uwiano wa ruwaza
4. Uasilia

4.1.2.1 Uwezekano wa kubashirika

Hyman (1975:91) anaeleza kwamba lazima kuwe na uwezekano wa kubashiri ni muundo ndani upi unaoweza kujitokeza kutokana na muundo nje katika neno hasa kwa kuzingatia mazingira ya kipasho husika. Kwa mfano katika Kiswahili, mifanyiko fulani hutabirika kutokana jinsi maneno ya aina moja huweza kudhihirisha aina moja ya badiliko kama vile nomino katika ngeli ya kwanza hudondosha /u/ ya kiambishi ngeli {mu} katika muundo nje wa nomino hizo. Matalani /mu+tu/ [mtu], /mu+geni [mgeni] na maneno mengine kama hayo.

4.1.2.2 Iktisadi ya vipashio

Katika uchanganuzi wa kifonemiki, uwasilishi wa kifonolojia huchukuliwa kuwa na iktisadi hasa ikitumia vipashio vichache vya kifonolojia. Wazo hili huchangia pakubwa kwa uwazi wa uwasilishaji unaosisitizwa katika FZA. Kwa mfano tunaporejelea maneno kama /**wa+itu**/ au /**wa+alimu**/, yanaweza kuandikwa kwa vipashio vichache kama [**wetu**] na [**walimu**] mtawalia.

4.1.2.3 Uwiano wa ruwaza

Kunazo ruwaza za sauti zisizokubalika na zinazokubalika katika lugha mbalimbali. Kwa mfano, sauti zilizonazalishwa hazipatikani katika mianzo ya maneno katika Kiingereza. Ruwaza hizi hueleweka kwa kila mzawa wa lugha.

4.1.2.4 Uasilia

Hyman (1975) anasema kwamba kuna kanuni za kifonolojia zinazojitokeza kila mara katika lugha mahususi. Hii ni kwa sababu mifanyiko hiyo hurahisisha matamshi. Kanuni hizo humwezesha mtu kutambua miundo ndani kwa kupitia miundo nje na kanuni za kifonolojia zinazohusika hujitokeza katika maneno mengi ya lugha hiyo. Maneno yanastahili kudhihirisha uasilia wa kifonetiki katika uwasilishaji wake ili kusahilisha matamshi. Kwa mfano, Hyman (1975) anasema kwamba ni rahisi kupata vipasuo vikidhoofika na kuwa vizuiwa kwamizwa vikiwa kati ya vokali kuliko

vizuiwa kwamizwa kuimarika na kuwa vipasuo vikiwa katika mazingira ya katikati ya vokali.

Schane (1973) anaziainisha sheria asilia katika vitengo vitatu. Sheria zenyewe ni za usilimisho (uwiano), sheria za muundo mwafaka wa silabi na sheria za kutengana kwa sauti iwezekanavyo. Kwa kuwa lugha hutofautiana kwa njia mbalimbali, mabadiliko yanayotokea pia hayafanani kikamilifu kwa kutegemea mazingira ya kimofonolojia katika lugha husika. Hata hivyo tutashughulikia sheria asilia kama anavyoeleza Hyman (1975) kuwa sheria hizi zina sifa za ubia kutokana na hali kwamba zinahusiana na fonetiki. Zaidi ya hayo ni kwamba sheria hizi zinapatikana mara kwa mara katika lugha nyingi au hata zote ulimwengu.

4.1.3 Mifanyiko ya kimofonolojia ya irabu

Tutashughulikia mifanyiko minne ya irabu za Kiolusuba na Kiswahili.

4.1.3.1 Udondoshaji wa irabu

Mfanyiko huu unahusishwa sana na muundo mwafaka wa silabi. Haya ni kwa mujibu wa Schane (1973). Katika baadhi ya lugha za kibantu mathalani Kiswahili Sanifu, hali hii ya kudondosha irabu hutokea wakati ambapo irabu imetanguliwa na irabu nyingine au inapotanguliwa na konsonanti katika mofu ya kiambishi ngeli na kufuatwa na konsonanti nyingine. Mfanyiko huu aghalabu hutokea katika nomino za ngeli 1, 2 na ya 3 katika viambishi vya upatanifu vya vitenzi na vivumishi katika ngeli mbalimbali. Mifano ya mfanyiko huu katika Kiswahili ni:

	Nomino	Mnukuu
76. Ngeli 1	/mu+tu/	[mtu]
Ngeli 2	/wa+alimu/	[walimu]
Ngeli 3	/mu+ti/	[mti]

Vivumishi

Vivumishi vina upeo mkubwa wa udondoshaji kuliko aina nyingine za maneno.

77. Shadda la /a/ + /a/ → /a/

/wa+akɔ/ [wako]

/ja+angu/ [jangu]

Shadda la /i/ + /ɛ/ → /ɛ/

/zi+ɛnu/ [zɛnu]

/li+ɛɲɛwɛ/ [lɛɲɛwɛ]

Shadda la /a/ + /ɛ/ → /ɛ/

/wa+ɛɲɛsi/ [wɛɲɛsi]

/wa+ɛma/ [wɛma]


Shadda la /i/ + /ɔ/ → /ɔ/

/li+ɔtɛ/ [lɔtɛ]


/hi+zi+ɔ/ [hizɔ]

Katika mifano tuliyoitoa tunaona kuwa irabu ya kwanza katika shadda ndiyo hudondoshwa na ile ya pili hubaki. Udondoshaji upo katika Kiolusuba katika vivumishi vya ngeli mbalimbali hasa vivumishi vimilikishi kuliko aina nyingine za maneno. Irabu hudondoshwa ili kusahilisha matamshi aghalabu mahali penye shadda la irabu. Kwa mfano:

	Mnukuu	maana
	Shadda la /a/+a/ → /a/	
78.	/ama+aŋgi/ [amaŋgi]	mengi
	/wa+aŋge/ [waŋge]	wangu



	Shadda la /a/+ɛ/ → /ɛ/	
79.	/wa+ɛɲɛnɛ/ [wɛɲɛnɛ]	peke yake
	/wa+ɛruguru/ [wɛruguru]	wa juu



Shadda la /a/+ /i/ → /i/


Nomino za ngeli ya sita ndizo aghalabu husheheni mfanyiko wa udondoshaji unaohusisha sauti /a/ na /i/. Nomino za ngeli hii ni za aina mbili. Kuna nomino ambazo zina kiambishi ngeli {eri-} katika hali ya umoja ambayo hupatikana katika ngeli ya tano. Aina ya pili za nomino za ngeli ya sita ni zile zisizochukua kiambishi cha ngeli katika hali ya umoja. Mifano ya nomino iliyo na kiambishi {eri-} katika hali zake za umoja ni:

Nomino		Mnukuu	maana
80. /eri+ino/	/ama+i+sɔ/	[ami:sɔ]	macho
/eri+ino/	/ama+i+nɔ/	[ami:no]	meno
/eri+ina/	/ama+i+na/	[ami:na]	majina


Aidha, kuna vivumishi mbalimbali katika Kiolusuba vinavyoonyesha mfanyiko wa aina hii kwa kuwa vina aina ya udondoshaji unaohusu sheria zaidi ya moja . Katika mfanyiko huo, irabu hudondoshwa kisha irabu inayotanguliza mzizi hurefushwa na kuchukua nafasi ya irabu iliyodondoshwa. Kwa mfano:

vivumishi	Mnukuu	maana
81. /awa+i+fu/	[awi:fu]	wetu
/ga+i+fu/	[gi:fu]	yetu
/ga+i+ju/	[gi:ju]	yenu

Kuna mifanyiko miwili katika maneno haya.




Kanuni yake ni:




Nomino zisizochukua kiambishi cha ngeli katika umoja hutokea ifuatavyo katika hali yake ya wingi.


82. / $\Phi+i+\eta$ ana/	/ama+i+ η ana/	[ama η ana]	maneno
/ $\Phi+i+gi$ /	/ama+i+gi/	[amagi]	mayai
/ $\Phi+i+saka$ /	/ama+i+saka/	[amasaka]	vichaka
/ $\Phi+i+toke$ /	/ama+i+ $t\text{ɔ}k\epsilon$ /	[amat $\text{ɔ}k\epsilon$]	ndizi



Shadda la /a/+ ɔ / \rightarrow / ɔ /

83. /wa+ ɔ na/	[w ɔ :na]	wote
/ga+ ɔ na/	[g ɔ :na]	yote(ngeli ya sita)






Hata hivyo, kuna vimilikishi katika nafsi ya pili na ya tatu visivyodhihirisha udondoshaji wa irabu na hivyo huishia kuwa na mkururo wa irabu. Kwa mfano,

Nomino	Mnukuu	maana
84. /wa+aε/	[wa:ε]	wake
/ja+aɔ/	[ja:ɔ]	yao
/wi+aε/	[wiaε]	vyake

Aidha kuna udondoshaji wa irabu inayotanguliza nomino wakati ambapo nomino imebadilishwa na kutumika kama mahali katika ngeli ya 9 na 10. Kwa mfano:

Nomino	Mnukuu	maana
85. /mu+enswa/	[munswa]	ndani ya nyungu
/mu+εsuku:li/	[musuku:li]	shuleni
/mu+εɲumba/	[muɲumba]	nyumbani
/ku+ɔmutwε/	[kumutwε]	kichwani

$\left. \begin{array}{l} \varepsilon \\ \text{ɔ} \end{array} \right\} \longrightarrow \phi / /u/ \text{ — } [+kons]$



Hata ingawa mfanyiko huu upo katika lugha hizi mbili, hautokei kwa upeo sawa kabisa. Ukweli ni kwamba upo katika Kiswahili katika kutamka baadhi ya nomino katika ngeli ya 1, 2 na 3. Hata hivyo kuna maneno katika Kiswahili ambayo yamehifadhi sauti /u/ ya kiambishi.

Kwa mfano:

86. /mu + umini/	[mu:mini]
------------------	-----------

/Mu + umbu/	[mu:mbu]
/mu + ujizu/	[mu:jizu]

Katika Kiolusuba /u/ ya kiambishi {mu} haidondoshwi katika nomino za ngeli ya 1,2 na 3. Mifano ya nomino katika Kiolusuba ni kama:

<i>Ngeli 1</i> Nomino	mnukuu	maana
87. /ɔmu + kazi/	[ɔmukazi]	mke
/ɔmu + sa:za/	[ɔmusa:za]	mume
<i>Ngeli 2</i>		
88. /awa + ana /	[awa:na]	watoto
/awa + ala/	[awa:la]	wasichana
/awa:mi/	[awa: mi]	viongozi
<i>Ngeli ya3</i>		
89. /ɔmu+ti/	[ɔmuti]	mti
/ɔmu+twɛ /	[ɔmutwɛ]	kichwa
/ɔmu+siri/	[ɔmusiri]	shamba

Mfanyiko huu hutokea ili kusahilisha matamshi. Haya tunasema kwa sababu katika mifano ya Kiswahili inaonyesha muundo mwafaka wa maneno kama vile /mu + tu/ /mu + ke/ lakini irabu inadondoshwa ili kupata muundo **KKI** kwa mfano [mtu] . Mifano ya ngeli ya pili ya Kiolusuba inayoonyesha kutodondoshwa kwa irabu na kuwa na muundo wa **KII** kwa kuwa irabu mbili zinafuatana . Kwa mfano [awa:na]. Tunaona Kiswahili kimebadilika pakubwa kwa kudondoshwa kwa irabu /u/ ya kiambishi {mu} katika nomino zake za ngeli ya 1 na pia kudondoshwa kwa /u/ ya mzizi wa nomino katika ngeli ya 3. Kiolusuba kimehifadhi maneno hayo bila kudondosha irabu. Kudondoshwa kwa irabu hata hivyo hudhihirika kwenye baadhi ya vivumishi na vimilikishi kama tulivyoonyesha awali.


4.1.3.2 Mvutano wa irabu

Mvutano wa irabu ni mfanyiko unaohusu sauti mbili za irabu kuungana na kuleta sauti mpya ya katikati. Aghalabu irabu moja huwa ya juu ilhali nyingine ni ya chini. Sauti ya juu huvutwa chini kidogo na ile ya chini kuinuliwa kidogo pia. Matokeo yake ni kwamba sauti itakayotokea si ya chini wala ya juu bali ni ya katikati. Sauti zile zinazovutana huishia kutupiliwa mbali. Maneno mengi huonyesha mfanyiko huu katika Kiswahili. Kwa mfano:

90. /ma+ino/	[mɛno]
/wa+iŋgi/	[wɛŋgi]
/wa+itu/	[wɛtu]
/ja+itu/	[jɛtu]

Katika mfanyiko huu, irabu /i/ ya [+juu] huvutwa chini na kuwa [-juu] /ɛ/ na irabu ya chini na [+nyuma] huletwa mbele na kuwa [-nyuma] /ɛ/. Sauti hizo zinazovutana hudondoshwa na badala yake sauti /ɛ/ hutokea.

Sheria yake ni: /a/ ↔ /i/ → [ɛ]



Inaelekea kwamba mfanyiko huu unaohusisha /a/ na /i/ katika hali ya mvutano na kuleta sauti /ɛ/ haupo katika Kiolusuba. Lugha ya Kiswahili ina mfanyiko huu ambao husababisha aghalabu sauti moja kupotea kabisa. Kulingana na utafiti huu, mfanyiko huu haupo katika Kiolusuba. Baadhi ya maneno yaliyo na sauti /a/ na /i/ katika ujirani huidondosha /i/ au hudondosha /a/ na kisha kuirefusha /i/. Kwa mfano nomino za ngeli ya 6 kamavile:

		maana
91. /ama+i+nɔ /	[ami:nɔ]	meno
/ama+i+ŋana/	[amaŋana]	maneno

Mfanyiko huu wa mvutano wa irabu ni wa muundo mwafaka wa silabi hasa inavyodhihirika katika Kiswahili. Hata ingawa haupo katika Kiolusuba, mfanyiko huo wa kurefusha irabu /i/ husahilisha matamshi licha ya kwamba silabi husalia katika muundo wa KII. Aidha, kuidondosha katika baadhi ya maneno pia huleta muundo mwafaka wa silabi. Kama anavyosema Lass (1984), mfanyiko unaotokea kutokana na athari za sauti moja kwa nyingine ni wa kutarajiwa. Kwa hivyo, mfanyiko huu wa mvutano wa irabu ni wa kutarajiwa

4.1.3.3 *Uyeyushaji*

Schane (1973) anasema kuwa mojawapo ya sababu za kuunda nusu irabu ni kule kuleta muundo mwafaka wa silabi. Nusu irabu huundwa wakati ambapo sauti ya irabu /u/ huimarika na kuwa nusu irabu /w/ au wakati ambapo irabu /i/ huimarika na kuwa /j/. Sauti hizo za irabu huhitaji nguvu kidogo katika kutamka zikilinganishwa na nusu irabu na hiyo ndiyo sababu ya kusema kuwa irabu hizo zinaimarika.

Anderson (1972) anaeleza kwamba uyeyushaji unaweza kutokea iwapo /u/ inafuatwa na [+irabu, -juu]. Mawazo haya yanasawiana na ya Schane kwamba mfanyiko huu huhusisha sauti /i/ na /u/ ambazo hubadilika na kuwa /j/ na /w/ inavyodhihirika katika maneno yafuatayo.

Kiswahili

Nomino

92. /mu+alimu/

/u+iŋgi/

Vivumishi

93. /mu+embamba/

/mu+izi/

/ku+etu/

/ku+aŋgu/

/i+etu/

Mnukuu

[mwalimu]

[wiŋgi]

[mwembamba]

[mwizi]

[kwetu]

[kwaŋgu]

[jetu]

Kiolusuba

Nomino

Ngeli 1

94. /ɔmu+ana/

/ɔmu+ɛru/

/ɔmu+ikɔ/

/ɔmu+ami/

/ɔmu+ala/

Ngeli 2

95. /ɔmu+ɔjɔ/

Ngeli 14

Kiolusuba

96. /ɔ+u+uɛru/

/ɔ+u+uiwi/

/ɔ+u+uami/

Mnukuu

[ɔmwana]

[ɔmwɛru]

[ɔmwikɔ]

[ɔmwami]

[ɔmwala]

[ɔmwɔjɔ]

mnukuu

[ɔwuɛru]

[ɔwuwiwi]

[ɔwuami]

maana

mtoto

safi

rafiki

mfalme

msichana

roho

maana

usafi

ubaya

uongozi

/ɔ+u+ulɔ:tu/ <i>vitenzi</i>	[ɔwulɔ:tu]	uzuri
97. /u+agɛnda/	[wagɛnda]	unaenda
/u+amala/	[wamala]	wamaliza


Vimilikishi

98. /u+angɛ/	[wangɛ]	wangu
/u+a:ɛ/	[wa:ɛ]	wake
/u+a:ɔ/	[wa:ɔ]	wao
/gu+angɛ/	[gwangɛ]	langu
/gu+a:ɛ/	[gwa:ɛ]	lake
/ku+a:ɛ/	[kwa:ɛ]	kwake
/ku+aɔ/	[kwa:ɔ]	kwako
/ku+angɛ/	[kwangɛ]	kwangu

Tunatambua kwamba uyeyushaji wa /u/ na kuwa /w/ unaweza kuwepo kwa sababu ya kufuatana kwa irabu mbili katika ujirani hasa /u/ na sauti nyingine ya irabu. Badala ya kudondosha irabu moja, irabu hiyo hubadilika na kuwa nusu irabu /w/.

$$/u/ \longrightarrow /w/ \text{ — } \frac{[\text{irabu}]}{\text{si } /u/}$$


Kanuni hii ni:



pia huundwa kutokana na kuyeyushwa kwa irabu /i/ katika kuunda vimilikishi hasa katika ngeli ya 4 na tisa. Kwa mfano:

Vimilikishi	Mnukuu	maana
99. /ɛ+i+a+jɔja/	[ɛjajoja]	imeandikwa
/ɛ+i+angɛ/	[ɛjangɛ]	yangu
/ɛ+i+a:ɛ/	[ɛja:ɛ]	yake
/ɛ+i+a:ɔ/	[ɛja:ɔ]	yako

$$\text{Sheria ya mabadiliko haya ni } /i/ \longrightarrow /j/ \text{ — } \frac{[\text{irabu}]}{\text{si } /i/}$$



Hata ingawa kufuatana kwa irabu huchangia sana kwa irabu hizo kuyeyushwa, tunapata kuwa hakuna uyeyushaji katika vimilikishi vya ngeli ya saba (7) na nane (8) licha ya kuwa vina mfuatano wa irabu katika miundo yake katika Kiolusuba. Kwa mfano

- | | | |
|-------------|-----------------------------|-----------------------|
| | | maana |
| 100. | Ngeli ya 7 [ɛkɪsusu ɛkɪaŋɛ] | sungura wangu |
| 101. | Ngeli ya 8 [ɛwisusu ɛwɪaŋɛ] | sungura wangu (wingi) |

Ni vigumu kuunda nusu irabu /j/ katika ngeli ya nane kwa kuwa itakuwa vigumu kutamka nusu irabu /w/ na /j/ kwa kufuatana. Nusu irabu /j/ huundwa katika baadhi ya maneno katika Kiolusuba hasa katika vimilikishi vya ngeli ya 4 na 9. Tumetambua kwamba mfanyiko huu unatokea katika Kiswahili na Kiolusuba. Motisha wake hasa ni kupata muundo mwafaka wa silabi. Ni mfanyiko unaotarajiwa kwa kuwa unatokea kutokana na mazingira ya irabu ya [+ juu] /i/ ikiwa katika mazingira ya kufuatwa irabu nyingine isipokuwa /i/ yenyewe.

4.1.3.4 Uwiano wa irabu

Huu ni mfanyiko ambao huonyesha namna athari za irabu moja hutokea kwenye irabu nyingine katika neno au maneno yanayopakana. Irabu hiyo hudhihirisha hali ya kufanana au kukaribiana kisifa na irabu iliyotangulia mathalani katika sifa bainifu kama vile hali ya mviringo, urefu na mahali pa kutamkwa kama vile nyuma au mbele. Katika uwiano wa irabu, vipashio vinaathiriana kisifa hata ingawa ni kwa mbali. Mfanyiko huu hudhihirika hasa katika mnyambuliko wa vitenzi kwa kauli tofauti tofauti mathalani ya kutendea na kutendesha. Irabu /i/, /a/ na /u/ katika mzizi ya vitenzi zinawiana na irabu /i/ katika viambishi vya kauli. Kwa mfano:

Kiswahili

Mzizi pig-

- 102.** Hali ya kutendea- /pig+ia/

Hali ya kutendesha- /fik+i ja/

Mzizi kul-

Kutendea /kul+ia/ → [kulia]
Kutendesha /li+fa/ → [liʃa]
Kutendeana /li+ʃana/ → [liʃana]

/i/ \
 /a/ ———> /i/
 /u/ /

Mifano mingine ni ile iliyo na /ɛ/ na /ɔ/ katika mizizi ya vitenzi vyake. Miundo ndani na miundo nje ya maneno yaliyoambishwa hutofautiana kwani /i/ hutokea kama /ɛ/. Irabu za vitenzi /ɔ/ na /ɛ/ zinaathiri kiambishi kifuatilizi na hivyo kutokea kama /i/.


Mifano ya uwiano huu ni:-

Mzizi let-

103. *Kutendea* /let+ɛ+a/ → [letea]
Kutendesha /tʃɛz+ɛ+ʃa/ → [tʃɛzɛ ʃa]
Kutendeana /let+ɛ+ana/ → [leteana]

Mzizi {tol-}

104. *Kutendea* /tol+ɛ+a/ → [toleɛa]
Kutendesha /tol+ɛ+ʃa/ → [toleʃa]



Kiolusuba		maana	
Kutenda	kutendea	kutenda	kutendea
105. [rɛ:ta]	[rɛ:tɛɾɛ]	leta	letea
[irana]	[iranra]	rudi	rudia
[jɔja]	[jɔjɛɾɛ]	andika	andikia
[rinda]	[rindra]	linda	lindia
[kuba]	[kubra]	piga	pigia
[fumba]	[fumbra]	pika	pikia
Kutenda	kutendana	maana	
106. [irana]	[iranana]	rudi	rudiana
[jɔja]	[jɔjanɛ]	andika	andikiana
[rinda]	[rindana]	linda	lindiana

[re:ta]

reetana

leta


leteana

Uwiano huu unadhihirika kwenye irabu katika mizizi ya vitenzi ambavyo huwiana na irabu katika viambishi vifuatili. Kwa mfano mzizi wa [a], [i] na [u] zinawiana kiasi kwamba fonimu hizo hudhihirika kwenye viambishi vya kauli ya maneno kutokana na sifa zake [+kaze]. Kwa mfano, neno kama vile [kubra] → [kubrana]. /u/ ya mzizi hutokea kama /a/ kwenye kiambishi cha kauli. Fonimu hizo zote ni [+kaze] zinakubaliana vile vile. [ɔ] kwenye mzizi hufuatwa na [ɛ] kwenye kiambishi kifuatili kutokana na sifa ya [-kaze]. Mzizi ukiwa na irabu ya [-kaze], viambishi vya kauli vilevile huchukua alofoni iliyo na sifa ya [-kaze]. Kwa mfano: /jɔjɛɛ/

/re:tɛɛ/

Kanuni yake ni:

/ɔ/ → /ɛ/ au



Hata hivyo mfanyiko huu ni dhahiri katika Kiswahili kuliko jinsi ilivyo katika Kiolusuba. Aidha, Kiswahili hunyambua maneno na kupata kauli nyingi zisizopatikana katika Kiolusuba. Wakati ambapo tunapata kauli za kutenda, kutendea, kutendesha, kutendeanana, kutendeka na kadhalika katika Kiswahili, Kiolusuba kinadhihirisha kauli chache tu kama vile kutenda, kutendea na kutendeanana.

108. /ni+umba/	[njumba]	[numba]
/ni+ungu/	[njungu]	[nungu]

Kiolusuba na Kiswahili zote zina mabadiliko ya ukaakaishaji. Hata hivyo si vipashio vyote vinavyokaakaishwa katika Kiswahili ndivyo vinavyokaakaishwa katika Kiolusuba. Vipashio visivyo vya kaaka gumu hutamkwa kwenye kaaka gumu katika mfanyiko huu.

b. Ukaakaishaji katika Kiolusuba

Ukaakaishaji unaohusu /k/ na /i/ haupo katika Kiolusuba. Kwa hivyo maneno yake katika ngeli ya saba husalia jinsi yalivyo katika muundo ndani na miundo nje.

Vuvumishi		mnukuu	Maana
109. /ki+angε/	→	[kiangε]	changu
/ki+a:ε/	→	[kia:ε]	chake
/ki+ɔ:na/	→	[kiɔ:na]	chote

Ukaakaishaji unaohusu /n/ na /i/ katika Kiolusuba


Katika Kiolusuba, mfanyiko huu upo katika maneno machache katika ngeli ya 9 na 10. Sauti ya nazali /n/ inayotolewa kwenye ufizi huletwa katika kaaka gumu kwa sababu ya ujirani wake na sauti /i/ ambayo inakaakaishwa na kuwa /j/. Kuna usilimisho mbele ambapo /n/ husilimiswa na /j/ na kutokea kama /j/.

110. /ε+ni+umba/	→	[εnjumba]	→	[εnumba]	nyumba
/ε+ni+ama/	→	[εnjama]	→	[εnama]	nama
/i+ni+uε/	→	[injue]	→	[ijue]	yenu
/ɔ+ni+ua/	→	[ɔnjua]	→	[ɔjua]	kunywa
/ni+za/	→	[njiza]	→	[niza]	naja
/ε+ni+jngi/	→	[εnjingi]	→	[εpingi]	nyingi

Ukaakaishaji ni mojawapo kati ya mifanyiko ya kifonetiki na hivyo hutarajiwa. Tunaona athari ya ujirani au kupakana kwa baadhi ya sauti na hivyo kupata kipashio kipya.

Kanuni yake ni:

$/n/ \longrightarrow [n] / \text{---} /i/ , [irabu]$
 si/i/



4.1.4.2 Usilimisho pamwe wa nazali

Badiliko hili hutokea wakati ambapo konsonanti ya nazali hufuatwa na konsonanti nyingine isiyokuwa ya nazali. Konsonanti hiyo ya nazali hubadilisha mahali pake pa kutamkiwa na kutamkwa katika sehemu sawa na konsonanti hiyo inayofuata. Foley (1977) anasema kuwa elementi zilizo dhaifu husilimishwa na zile zilizo na nguvu zaidi. Schane (1973) anaieleza kanuni hii kama kanuni ya uwiano yaani mkubaliano wa nazali na kitamkwa kinachofuata kwamba ni wapi zitakapotamkwa. Mfanyiko huu unapatikana katika ngeli ya 9 na 10.

Kuna aina mbili za usilimisho. Usilimisho mbele na usilimisho nyuma. Katika usilimisho mbele, sauti inayofuata huathiri sauti iliyotangulia ilhali usilimisho nyuma ni hali ambapo sauti ya mbele au iliyotangulia huathiri sauti inayofuata. Mifano ya maneno yenye sauti iliyosilimishwa ni:

Kiswahili


111. /N+gɔmbɛ/ [ŋɔmbɛ]
 /N+vua/ [ŋvua]
 /N+biŋgu/ [mbiŋgu]

Kiolusuba

Ngeli 9/10	mnukuu	maana
112. /εN+vula/	[εɲvula]	mvua
/εN+buzi/	[εmbuzi]	mbuzi
/εN+zovu/	[εnzovu]	ndovu
/εN+gɔkɔ/	[εngɔkɔ]	kuku
/εN+lɔ:tu/	[εndɔ:tu]	nzuri
/εN+bwa/	[εmbwa]	mbwa
/εN+tikiri/	[εntikiri]	punda

Maneno yanayoonyesha mfano wa usilimisho mbele ni [εmbuzi] na [εɲvula] kwa kuwa mtu anapotamka [sauti] /N/ huwa tayari kutamka /b/ kwa hivyo /b/ huvuta /N/ na kutokea kama /mb/ ambayo ni sauti ya [+midomo]. Vivyo hivyo /v/ husilimishwa na kuwa /ɲ/ ambayo pia ni [+midomo]. Mifano ya maneno yanayoonyesha usilimisho nyuma ni kama vile [εngɔkɔ] na [εnjugu] ambapo sauti /n/ ya mbele huvutwa mbele na sauti ya kaaka laini na sauti kaaka gumu na kutamkia kama [ɲg] na [ɲj]. Hata hivyo kuna sauti ambazo hazikubadilisha mahali pa kutamkia kama inavyodhihirika kwenye mifano tuliyoitoa. Maneno kama vile [εntiriki] na [εndɔ:tu]. Maneno hayo yana sauti zinazosilimishwa yakitokea katika sehemu sawa ya kutamkia kwa hivyo sauti hizo huungana tu ili kusahilisha matamshi.

Kanuni hii inaweza kuelezwa hivi.



Katika lugha hizi mbili, kanuni ya usilimisho unatokea sawia. Pia tunasema kwamba ni badiliko ambalo linatabirika kutokana na sababu kwamba sauti moja huathiri nyingine. Pia ni mfanyiko wa kutarajiwa katika lugha hizi zote kwa sababu hupata motisha kifonetiki

4.1.4.3 Kuimarika kwa konsonanti

Schane anaeleza kanuni hii kama kanuni ya kiasilia ya usilimisho mbele. Wanaouunga mkono wazo hili ni pamoja na Mgullu (1999) na Iribemwangi (2010). Katika lugha nyingi za kibantu, mfanyiko huu huhusu, likwidi /l/ na /r/. Dhana ya kuimarika inarejelea hali ya sauti ambayo kwa kawaida hutamkwa kwa nguvu kidogo kubadilika na kuwa ya kutamkwa kwa nguvu nyingi.

Nguvu za sauti hudidimia kutoka kwa vipasuo vikielekea kwa vizuiwa kwamizwa, vikwamizwa, nazali, likwidi, nusu irabu na mwishowe irabu. Kudhoofika huku kunazingatiwa pia na hali ya mghuno. Kwa mfano sauti za vipasuo zisoghuna zinahitaji nguvu nyingi kuliko zile ghuna.

Kielelezo 4.2 Kuimarika kwa konsonanti

	Sighuna	ghuna
Vipasuo	1	2
Viz- kwamizwa	3	4
Vikwamizwa	5	6
Nazali		7
Likwidi		8
Nusu- irabu		9
Irabu		10

Sauti zinazochukua nafasi ya 1 ni zile zinazohitaji nguvu zaidi ambazo ni vipasuo visoghuna zikifuatwa na zile za nafasi ya 2 ambazo nia vipasuo ghuna. Nafasi ya tatu ni ya vizuiwa vikwamizwa kisha vikwamizwa ambazo sighuna. Nafasi ya tano ni ya sauti zisoghuna za vikwamizwa zikifuatwa nazile ghuna. Nazali zinapatikana katika nafasi ya saba kisha likwidi hufwata. Kwa hivyo sauti zilizodhaifu zaidi ni zile za irabu. Kutokana na hali hii, iwapo mfanyiko utatokea unaobadilisha sauti fulani kiasi

cha kupata sifa za sauti inayohitaji nguvu zaidi ili kutamka , sauti hiyo itakuwa imeimarika. Kwa mfano :

Kiswahili	mnukuu
113. /N+limi/	[ndimi]
/N+lɔɔ/	[ndɔɔ]
/N+rɛfu/	[ndɛfu]
/N+lɔa/	[ndoa]
/N+refu/	[ndɛfu]
/N+wili/	[mbili]

Kiolusuba

Katika Kiolusuba mfanyiko huu hutokea katika baadhi ya maneno katika ngeli ya 9/10.


Nomino	mnukuu	maana
114. /eN + la/	[enda]	tumbo
/eN + rerema/	[enderema]	aina ya mboga


Vivumishi

Kiolusuba	maana
115. /ɛN+lɔ:tu/	[ɛndɔ:tu] nzuri
/ɛN+lala/	[ɛndala] moja
/ɛN+wi:wi/	[ɛmbiwi] mbaya

Vipashio vya likwidi, kitambaza /u/ na kimadende /r/ vimeimarika na kuwa vipasuo /d/. Nusu irabu /w/ imeimarika na kuwa kipasuo /b/. Sauti /r/, /l/ na /w/ ambazo ni [+ vifulizwa] zinakuwa [– kifilizwa]. Kwa sababu ya athari ya /N / kwa sauti hizo nyingine, mfanyiko huu ni wa kutarajiwa

Tumeona mabadiliko ya aina tatu hapa yaani /l/ kuimarika na kuwa /d/, /r/ kuimarika na kuwa /d/. Pia /w/ kubadilika na kuwa/b/. Fonimu /l/ na /r/ ni za likwidi na /w/ ni nusu irabu. Zote zimepata kuimarika hadi kuwa vipasuo ghuna. Sheria hii huonyeshwa hivi:





4.1.4.4 Kudhoofika kwa konsonanti

Sauti hudhoofika wakati sauti inayohitaji nguvu nyingi kutamka hubadilika na kuwa sauti inayohitaji nguvu kidogo kuliko ilivyokuwa awali. Hali hii hutokea wakati wa unominishaji wa vitenzi katika lugha nyingi za Kibantu kama anavyosema Polome (1976). Mifano ni:

Kiswahili


116. [penda]	/mu+pendi/	[mpenzi]
[suka]	/mu+suki/	[msusi]
[fuata]	/mu+fuati/	[mfuasi]
[lapa]	/mu+lapi/	[mlafi]

Kiolusuba

117. [ɔmu+lɔnda]	[ɔmulɔnzi]	maana	mfuasi
------------------	------------	-------	--------

	[ɔwulɔnzi]	ufuasi
[ɔmu+rindi]	[ɔmurinzi]	mlinzi
	[ɔwurinzi]	ulinzi
[ɔmu+gonga]	[ɔmugɔnzi]	mpendwa
[ɔmu+gibi]	[ɔmugizi]	mzawa wa mahali

Kanuni ya mfanyiko huu ni:



Katika sehemu hii tulishughulikia mifanyiko ya kifonolojia yanayotokea katika Kiswahili Sanifu na Kiolusuba. Mifanyiko tuliyoionyesha ni; kudondoshwa kwa irabu, kuyeyushwa kwa irabu, na kukubaliana kwa irabu. Kwa upande wa konsonanti, tulishughulikia kudhoofika kwa fonimu, ukaakaishaji na usilimisho pamwe wa nazali. Kama anavyosema Hyman (1975) mifanyiko hii imeonyesha hali ya kuweza kutarajiwa hasa zile zinazopata motisha kifonetiki.

4.2 Hitimisho

Katika sehemu hii, tumeshughulikia mifanyiko saba ya kifonolojia. Tulipata kwamba mifanyiko hiyo inadhihirika katika lugha hizi mbili japo kwa viwango na mawanda tofauti tofauti kama vile katika nomino, vivumishi, vimilikishi na mengineyo. Pia, tumeona kuwa lugha zote mbili zina mifanyiko ya kutarajiwa na isiyotarajiwa. Mifanyiko ya kutarajiwa ni ile inayosababishwa na mazingira ya kifonetiki kama vile ukaakaishaji ilhali mifanyiko isiyotarajiwa ni ile ile isiyosababishwa na mazingira ya kifonetiki kama vile kudondosha irabu ili kusahilisha matamshi. Tunalotaka kusisitiza

ni kwamba ni kweli kila lugha asilia ina sifa zake zisizoweza kuhamishwa na kulazimishwa katika lugha nyingine. Kwa mfano katika kudondoshwa kwa /u/ na /a/ katika ngeli ya kwanza na ya pili, Kiswahili kinadhihirisha mfanyiko huo katika nomino zake ilhali Kiolusuba hakina mfanyiko huo katika nomino zake ambazo wakati mwingine zina miundo ndani na maana sawa na nomino zilezile za Kiswahili. Aidha katika ukaakaishaji katika ngeli ya saba, Kiswahili na Kiolusuba zina miundo ndani sawa katika baadhi ya maneno lakini tunapata miundo nje tofauti kabisa. Kwa mfano:

- 118.** Kiswahili /ki+angu/ → [tʃangu]
Kiolusuba /ki+angε/ → [kiangε]

5. SURA YA TANO

5.1 ATHARI ZA KIMOFOFONOLOJIA

5.1.1 Utangulizi

Kwa kuwa tumeshashughulikia masuala mbalimbali kama vile mifumo ya fonimu, miundo ya silabi na hata mifanyiko ya kifonolojia ya Kiswahili na Kiolusuba, katika sura hii tunaangazia athari zinazothahirika kimatamshi miongoni mwa wazungumzaji wa Kiolusuba wanapotumia Kiswahili. Aidha, tunaeleza sababu ambazo zinachangia kutokea kwa hali hizo. Tutaonyesha mifano ya baadhi ya maneno yanayoonyesha kuwepo kwa athari pamoja na maumbo sahihi ya maneno yanayonuiwa kutamkwa na wazungumzaji hao. Aidha maneno hayo hudhihirisha kutozingatia mfumo wa sauti za Kiswahili katika matumizi yake. Kiswahili kina mfumo wa sauti mahususi ambao unastahili kufuatwa ili kukitumia kwa usahihi. Kila lugha huwa na miundo ya maneno inayoruhusiwa kama vile sauti zipi zinazoweza kufuatana na zipi katika mazingira fulani. Iwapo mtumizi wa lugha ya Kiswahili atazihamisha sauti za lugha yake ya kwanza, ataivuruga Kiswahili na hivyo kukitumia vibaya.

Nadharia ya FZA inatufaa kwa kuwa ndiyo itatuongoza katika kupambanua miundo sahihi ya lugha hizi mbili na pia ndiyo itatuwezesha kueleza visababishi vya kila aina ya athari inayodhihirika.

Aghalabu athari hizo huzua utata wa maana hasa ikiwa fonimu husika inapatikana katika lugha zote mbili. Pia, maana huweza kupotea kabisa. Matatizo ya kimatamshi hayadhuru sana sauti za irabu ila mara chache wazungumzaji husikika wakirefusha baadhi ya vokali katika matumizi ya Kiswahili. Kwa mfano, mtu anaweza kusema *chaai* badala ya chai. Hali kama hii hutokea kwa sababu irabu zote za Kiswahili zinapatikana katika Kiolusuba lakini irabu ndefu katika Kiolusuba hazipo katika Kiswahili. Athari za mofofonolojia ya Kiolusuba katika matumizi ya Kiswahili husababishwa na sauti za Kiswahili zisizopatikana katika Kiolusuba na miundo tofauti ya baadhi ya maneno. Sauti hizo hutamkwa vibaya au wakati mwingine hundoshwa kabisa. Athari zinazotokana na data yetu ni:

5.1.2 Athari katika matumizi ya /h/

Baadhi ya wazungumzaji wa Kiolusuba huchopeka sauti /h/ au huidondosha katika baadhi ya maneno na kisha kupata miundo isiyo sahihi. Kwa mfano:

mifano	umbo sahihi
119. ana	[hana]
asubui	[asubuhi]
serekea	[ʃɛɾɛhɛkɛa]
akika	[hakika]
hasubui	[asubuhi]
hasante	[asantɛ]

Sababu

Katika Kiolusuba, hakuna fonimu /h/. Hali hii inasababisha wengi kutamka maneno yenye sauti hii kwa kuidondosha au kuichopeka pasipostahili hasa miongoni mwa wanafunzi wanaojifunza Kiswahili kama lugha ya pili. Hii ni kwa sababu wengi huchanganyikiwa na kukosa kujua waitumie sauti hiyo wapi.

5.1.3 Athari katika matumizi ya /ð/

mifano	umbo sahihi
120. zambi	[ðambi]
zarau	[ðarau]
azuuri	[aðuhuri]
zairi	[ðahiri]

Sababu

Fonimu /ð/ hutamkwa kwa ulimi na meno. Kiolusuba hakina sauti ya meno na ulimi kama /ð/ kwa hivyo sauti /z/ ambayo ni ghuna kama ilivyo / ð/ ndiyo hutamkwa badala yake. Sauti /z/ hutamkwa wakati bapa la ulimi hukaribiana sana na kaaka gumu na huku hewa ikipitishwa kwa mkwamzo kandokando mwa ulimi na kusababisha mkwaruzo. Ala hizo husika ndizo zinakaribiana na za kutamka sauti /ð/. Kwa hivyo, mzungumzaji wa Kiolusuba hutumia /z/ ambayo hukaribiana na /ð/ kwa kiasi fulani.

5.1.4 Kubadilisha /ɾ/ na /g/

mifano	umbo sahihi
121. agalabu	[avalabu]

luga	[luva]
gala	[ɣala]
gali	[ɣali]
gasia	[ɣasia]
gorofa	[ɣorofa]
gafla	[ɣafla]

Sababu ya athari

Sauti /ɣ/ haimo kwenye mfumo wa sauti za Kiolusuba. Kwa hivyo, sauti /g/ ambayo pia hutamkiwa kwenye kaaka laini huchukua nafasi ya /ɣ/ wanapotumia Kiswahili. Sauti hizo mbili hutamkiwa kwenye sehemu sawa ya kinywa ingawa moja ni ya kipasuo ilhali nyingine ni kikwamizwa. Maana hupotea katika hali hii. Hata hivyo maana wakati mwingine haipotei hasa anayezungumziwa akielewa jinsi mtumizi huyo wa Kiswahili anavyohamisha mfumo wa sauti za lugha yake ya kwanza.

5.1.5 Matumizi ya /s/ badala ya /ʃ/

mifano	umbo sahihi
122. soka	[ʃoka]
sika	[ʃika]
swari	[ʃwari]
samba	[ʃamba]

Sababu ya athari

Athari hii hutokea kwa sababu fonimu /ʃ/ haipatikani katika Kiolusuba. Sauti /ʃ/ hutamkiwa kwa kupitisha hewa kwenye meno ya mbele yakiwa yamegusana huku bapa la ulimi ukiwa umekazwa. Kikwamizwa kilicho karibu kimatamshi ni /s/ inayotamkiwa kwa kupitisha hewa kando kando mwa ulimi huku ncha ya ulimi ikiwa imegusana na ufizi. Hewa hupitishwa kwa mkwaruzo lakini /ʃ/ inayonuiwa hutokea kama /s/.

5.1.6 Matumizi ya /j/ badala ya /tʃ/

mifano	umbo sahihi
123. jini	[tʃini]
jupa	[tʃupa]
joo	[tʃoo]

nji	[nʃi]
mjana	[mʃana]

Sababu

Fonimu /tʃ/ haipatikani katika Kiolusuba na badala yake sauti /j/ iliyo ghuna na inayotamkiwa kwenye kaaka gumu kama ilivyo /tʃ/ ndiyo hutumika sana miongoni mwa wazungumzaji wa Kiolusuba wanapoitumia Kiswahili kama lugha ya pili.

5.1.7 Matumizi ya /s/ badala ya /θ/

mifano	umbo sahihi
124. sumni	[θumni]
semanini	[θemanini]
asari	[aθari]

Sababu ya athari

Mfumo wa fonimu wa Kiolusuba hauna sauti /θ/. Kwa hivyo mzungumzaji ambaye anazungumza Kiolusuba kama L₁ anapoitumia Kiswahili anaishia kudhihirisha athari za sauti nyingine katika kuitamka sauti hii. Sauti /θ/ ni ya ulimi na meno na si ghuna. Kwa hivyo sauti ya Kiolusuba ambayo si ghuna ni /s/ inayotamkwa wakati ncha ya ulimi na ufizi hukaribiana kisha kuruhusu hewa kupita kwa kukwamizwa. Hata hivyo, miongoni mwa wanafunzi wa shule hasa za msingi, sauti hii hutumiwa kimakosa kwa kubadilishwa na sauti /ð/. Kwa mfano wanafunzi wanaandika maneno kama haya:

adhari badala ya athari au
orodha badala ya orodha

5.1.8 Matumizi ya /k/ badala ya /x/

mifano	umbo sahihi
125. Takmisa	[taxmisa]
Sabalkeri	[sabalxeri]

Sababu

Sauti /x/ haipatikani katika Kiolusuba . Kwa hivyo, sauti hii hutamkwa kama /k/ na baadhi ya wazungumzaji wa Kiolusuba. Hii ni kwa sababu /k/ hutamkwa kwenye kaaka laini kama ilivyo /x/.

5.1.9 Uchopekaji wa irabu /u/

Kutokana na kazi yetu kuhusu mofonolojia ya Kiswahili na Kiolusuba, tumegundua kwamba kuna tofauti kati ya miundo ya maneno fulani. Tofauti hizo pia huathiri matumizi ya Kiswahili kwa kiwango fulani kimatamshi. Kwa mfano maneno ya ngeli ya kwanza na ya tatu.

mifano	umbo sahihi
126. mutu	[mtu]
mukurugenzi	[mkurugenzi]
mugeni	[mgeni]
muti	[mti]
mulima	[mlima]
mulango	[mlango]

Sababu

Katika Kiolusuba, sauti /u/ ya kiambishi haidondoshwi katika ngeli ya 1 na ya 3. Kwa mfano *omuti*, *omugeni* na mengineyo. Kwa hivyo, nomino za ngeli ya kwanza na ya tatu husalia na sauti hiyo. Wazungumzaji wa Kiolusuba hufanya makosa ya kuhamisha matumizi yao ya nomino za ngeli ya kwanza na ya tatu katika Kiswahili.

Kosa la uchopekaji wa sauti /u/ mwanzoni mwa neno

Kosa	umbo sahihi
127. uwoga	[woga]
uwizi	[wizi]
uwingi	[wingi]

sababu ya kosa

Tofauti na jinsi ilivyo katika Kiswahili ambapo maneno mengi huyeyusha /u/ na kuwa /w/ inapofuatwa na irabu nyingine isipokuwa /i/. Maneno mengi katika Kiolusuba huwa na /u/ pamoja na /w/ zikifuatana mtawalia. Kwa mfano:

Kiolusuba	maana
128. Ouwita	[ugali]
Ouwiiwi	[ubaya]

Kutokana na hali kwamba wazungumzaji wa Kiolusuba hutumia uainishaji wa nomino ngeli wa kimofolojia, maneno mengi ya Kiolusuba ambayo yana maana sawa na ya Kiswahili hupatikana katika ngeli tofauti. Kwa hivyo, wazungumzaji wa Kiolusuba huzingatia kiambishi awali tu katika kuunda sentensi na wanapohamisha matumizi haya katika Kiswahili, hu fanya makosa. Kwa mfano katika Kiolusuba wanasema.

129. Eng'ombe eyange	ng'ombe wangu
Embuzi eyange	mbuzi wangu
Ekisusu ekiange	sungura wangu
Entewe eyange	kiti changu


Hali hii huzua hali kwamba wazungumzaji wa Kiolusuba wanajumuisha maneno kutokana na viambishi awali. Mzungumzaji akijaribu kuhamisha kanuni za lugha yake ya kwanza katika Kiswahili hutokea kama makosa. Kwa mfano:

130. Chai changu	chai yangu
Kitabu kiangu	kitabu changu

Jadwali 5.1 athari katika kazi andishi

Shule	Uozi			Wakinga			Jumla	Asili Mia
	4	6	8	4	6	8		
Darasa	4	6	8	4	6	8		
<i>Idadi ya Wanafunzi</i>	5	5	5	5	5	5	30	100
Udondoshaji wa /h/	5	5	4	5	5	4	28	93.3
Uchopekaji wa /h/	5	5	3	5	4	2	24	80.0
Uchopekaji wa /u/	5	4	4	5	5	4	27	90.0
/j/ badala ya /t/	2	1	2	3	2	1	11	36.7
/g/ badala ya /s/	5	5	4	5	5	4	28	93.3
/z/ badala ya /ð/	4	3	2	3	3	1	16	53.3
/s/ badala ya /ø/	4	3	2	3	3	1	16	53.3
/s/ badaa ya /j/	5	4	3	5	4	4	25	83.3


Kielelezo 5.2 Baa grafu ya athari katika kazi andishi



Jadwali 5.3 athari katika matamshi

Shule	Uozi			Wakinga			Jumla	Asili Mia
	4	6	8	4	6	8		
Idadi ya Wanafunzi	5	5	5	5	5	5	30	100
Udondoshaji wa /h/	5	5	4	5	5	4	28	93.3
Uchopekaji wa /h/	5	4	3	5	4	4	25	83.3
Uchopekaji wa /u/	5	5	5	5	5	4	29	96.0
/j/ badala ya /tʃ/	4	3	2	3	5	3	20	67.7
/g/ badala ya /ɣ/	5	5	5	5	5	4	29	96.0
/z/ badala ya /ð/	4	3	2	3	3	2	16	56.7
/s/ badala ya /ə/	5	4	3	3	3	2	20	67.7
/s/ badaa ya /ʃ/	5	4	4	5	4	4	26	86.7

Kielelezo 5.4 Baa grafu ya athari katika kazi andishi



Majedwali haya na baa grafu zinaonyesha idadi ya wanafunzi walioathirika kimatumizi yaani kimatamshi na katika kazi andishi. Herufi U na W zinasimamia shule mbili, Uozi na Wakinga. Kila darasa lina wanafunzi watano. Baa grafu inaonyesha idadi ya wanafunzi walioonyesha kutatizika katika kila kitengo cha athari huku jedwali likionyesha asili mia ya athari katika madarasa husika yakijumuishwa.

5.2 Hitimisho

Katika sura hii tumeonyesha baadhi ya maneno yanayodhihirisha athari za kimofonolojia ya Kiolusuba katika matumizi ya Kiswahili. Aidha tumeleza visababishi vya athari hizo kutokana na tofauti mbalimbali za mifumo ya sauti na miundo ya maneno. Pia tumetumia majedwali pamoja na baa grafu kuonyesha viwango vya athari hizo.

6. SURA YA SITA

6.1 MATOKEO NA MAPENDEKEZO

6.1.1 Utangulizi

Katika sura hii tunatoa muhtasari wa utafiti wetu na pia mapendekezo kuhusu kazi hii kutokana na utafiti wetu na pia kwa manufaa ya tafiti zitakazofanywa baadaye.

6.1.2 Muhtasari wa matokeo

Utafiti huu ulijikita katika kujadili athari za mofofonolojia za Kiolusuba katika matumizi ya Kiswahili kama lugha ya pili. Athari hizo zimedhihirika katika viwango vya kifonolojia na mofolojia. Utafiti huu umetudhihirishia kwamba haipotesia zetu zina mashiko. Tulidai kwamba kuna tofauti kubwa baina ya mifumo wa fonimu za Kiswahili na Kiolusuba ambayo huathiri matumizi ya Kiswahili miongoni mwa wazungumzaji wa Kiolusuba. Katika sura ya pili tuliweza kulinganisha mifumo ya kifonolojia ya lugha hizi mbili na kuonyesha fonimu mbalimbali zisizopatikana katika kila lugha. Aidha tumeweza kuthibitisha kwamba athari hiyo ipo kutokana na makosa mengi tuliyoyaorodhesha.

Katika sura ya tatu, tumelinganisha mifano ya miundo ya silabi za Kiolusuba na za Kiswahili ambapo tulipata tofauti kidogo tu. Hata hivyo, tofauti hiyo pia imedhihirika kwamba huchangia katika athari hiyo. Aidha, tumelinganisha mifanyiko ya kifonolojia ya Kiswahili na Kiolusuba katika sura ya nne. Tumetambua kwamba mifanyiko hiyo pia hudhihirisha kiwango fulani cha athari za kimofonolojia za Kiolusuba kwa Kiswahili.

Haipotesia yetu ya mwisho ni kwamba kuna maneno mengi ya Kiswahili yanayoonyesha athari ya Kiolusuba kimatamshi miongoni mwa wazungumzaji wa Kiolusuba. Jambo hili pia tumelishughulikia katika sura ya tano.

Nadharia ya FZA ilitufaa sana katika kazi hii hasa katika kuchunguza miundo ndani na miundo nje ya maneno na jinsi sauti zinavyobadilika katika harakati za kutamka maneno katika lugha hizi mbili.

Utafiti wetu umebaini kuwa kazi ya aina hii kuhusiana na Kiolusuba haijafanywa kwa kuwa kuna uchukulizi kwamba lugha hii imedidimia na kwamba haina wazungumzaji

wengi. Utafiti huu umetambua kwamba Kiolusuba kina wazungumzaji wake asilia katika umri tofauti tofauti. Pia wazungumzaji hao huitumia lugha hii katika shughuli takriban zote za maisha yao.

6.1.3 Mapendekezo

Utafiti huu hauwezi kudai kwamba umeshughulikia athari za Kiolusuba katika matumizi ya Kiswahili kikamilifu bali ni matumaini yetu kwamba tafiti nyingine zitaweza kutalii masuala haya na mengine kama vile athari zinazotokana na tofauti za kisarufi baina ya lugha hizi mbili.

Ni matumaini yetu kwamba walimu wa shule zinazopatikana katika maeneo ambapo Kiolusuba huzungumzwa watatilia maanani mafundisho ya sauti kamili za Kiswahili hasa katika madarasa ya chini ili kuweka msingi thabiti kwa matumizi ya Kiswahili.

Aidha, tunapendekeza kwamba serikali na wataalamu wengine waweke sera imara ya kuhifadhi lugha zinazohofiwa kwamba huenda zikapotea. Kwa hivyo, ni matumaini yetu kwamba lugha ya Kiolusuba itawekwa kama somo la lazima katika madarasa ya chini ya shule za msingi katika maeneo ya Suba.

MAREJELEO

- Anderson, B. (1972) Mh. *Contributions to Generative Phonology*. University of Texas Press: Austin London.
- Ayot, H. (1973) *A History of the Luo Abasuba of Western Kenya 1790-1940*. Nairobi: KLB.
- Chomsky, N. and Halle, F. (1968) *Sound Patterns of English*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Corder, S. (1967) *Error Analysis and Interlanguage*. Oxford: Oxford University Press.
- Crystal, D. (1991) *A Dictionary of Linguistics and Phonetics*. New York: Bluckid Publishers.
- Foley, J. (1977) *Foundations of Theoretical Phonology*. Cambridge University Press: Cambridge.
- Guthrie, M (1947) *Comparative Bantu. An Introduction to Comparative Linguistics and Pre-History of Bantu Languages*. Gregg: Farnborough.
- _____ (1948) *Classification of Bantu Languages*. Oxford: Oxford University Press.
- Habwe, J. and Karanja, P. (2004) *Msingi Wa Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi. Phoenix Publishers.
- Hooper, J. (1976) *Introduction to Generative Phonology*. Oxford: Oxford University Press.
- Hyman, L (1975) *Phonology: Theory and A nalysis*. New York : Holt Rinehart and Row.
- Iribemwangi, P. (2010) *The Structure of Kiswahili Sounds, Sound changes and Words*. Saarbruken: Verlag
- Iribemwangi, and Mukhwana, A. (2011) *Isimu Jamii*. Nairobi. Focus Publishers.
- Jones, D. (1989) *An Outline of English Phonetics*: Cambridge. Cambridge University Press.
- Katamba, F. (1992) *An Introduction to Phonology*. Longman: London
- Kent, P. (1978) *Encyclopedia of Library and Information Science*. New York: Marcel Decker.
- Kihore, Y. Massamba, D and Matangila, M. (2001) *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: TUKI.
- Ladefoged, P. (1962) *Elements of Acoustic Phonetics*. London : University of Chicago Press.
- _____ (1967) *Phonetics*. New York: Oxford University.

- Lass, R. (1984) *Phonology. An Introduction to basic phonology*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Massamba, D. P. (1999) *Sarufi Miundo ya Kiswahili*. Dar-es-Salaam. TUKI.
- _____ (2004) *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*: Dar-es-Salaam. TUKI
- Mathews, P. (1974) *Morphology: An Introduction to the Theory of Word Structure*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Mattah, N. (2008) *Culture of the Abasuba*. Nairobi: Wycliff Bible Society
- Meinhorf, C. (1973) *Introduction to phonology of Bantu Languages*. Oxford: Oxford University Press.
- Mgullu, R.S (2001) *Mtalaa Wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Publishers.
- Ndungu, I. (1999) *Kikuyu Learners of English as Second language: PhD. Thesis*: Nairobi: UoN
- Ogechi, N. Oduor, J. and Iribemwangi, P(2012) Ed. *The Harmonization and Standardization of Kenyan Languages Chapters 2 and 5*. Cape Town: The Centre for Advanced Studies of African Society.(CASAS)
- Okombo, D. and Rottland, F. (1981) *African Languages. An Introduction*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Okombo, D. (2001) *Language and Ethnic Identity: The case of the Abasuba*. Kenya Journal of sciences.
- Osogo, J. N. (1971) *A Traditional History of Kenya: Teacher's Hand Book*. Nairobi: Longman Publishers.
- Polome, E. (1967) *Swahili Language Handbook*. Washington: Centre for Applied Linguistics.
- Rapando, M. (2005) *Makosa ya Kimfofo-sintaksia yanajitokeza katika Kazi za Kiswahili zilizoandikwa na Wanafunzi wa shule za Upili jijini Nairobi: Tasnifu ya M.A (UoN)*.
- Schane, S. (1973) *Linguistic Change and generative phonology*. Oxford: Oxford University Press.
- Selinker, L. (1969) *LanguageTransfer, General Linguistics*: New York: Rawlence Erlbaum Associates, inc. (RAL).
- Selinker, L. (1972) *Inter Language*. New York: Rawlence Erlbaum Associates, inc. (RAL)

Swaleh, R. H (2005) *Mofosintaksia ya Kishazi cha Kitiku: Mtazamo wa Uminimalisti*.
Thesis University of Nairobi

Wycliffe Bible Translators (2010) *Endagano Empia. The New Testament in the Suba language of Kenya: Bible Translation and Literacy* (E.A) Kenya.

VIAMBATISHI

KIAMBATISHI I: Maswali Ya Imla

Andika maneno haya kama unavyoyasikia

- 1.mtu
- 2.mpira
- 3.dhambi
- 4.nchi
- 5.kitabu changu
- 6.asubuhi
- 7.shida
- 8.ghala
- 9.sherehe
- 10.ghorofa
- 11.cherehani
- 12.theluji
- 13.rinda mpya

Andika sentensi hizi

- 14.Hiki ni kijani kibichi.
15. Shule yetu ni nzuri.
- 16.Nyumba ya ghorofa ni ipi?
- 17.Kitanda chake kimevunjika.
18. Alhamisi ni siku ya soko.
- 19.Watu hula wakati wa aduhuri.
- 20.Tulishikwa na woga.

KIAMBATISHI II: Maswali Ya Insha

1. Darasa la nne- Siku ya michezo shuleni
2. Darasa la sita – Ndoto ya kutisha
3. Darasa la nane- Ndoto ya kutisha